ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE PANDU AMEIR KIFICHO

1. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	Kuteuliwa na Rais
2. Mhe. Omar Othman Makungu	Mwanasheria Mkuu
3.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
4.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
5.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
6.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	Jimbo la Magogoni
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Jimbo la Mgogoni
8.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	Jimbo la Donge
10.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
11.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
12.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
13.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
14.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
16.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
17.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake
18.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
19.Mhe. Farida Amour Moh'd	Nafasi za Wanawake
20.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Kuteuliwa na Rais
21.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
22.Mhe. Haji Faki Shaali	imbo la Mkanyageni
23.Mhe. Haji Mwadini Makame	Jimbo la Nungwi
24.Mhe. Haji Omar Kheri	Jimbo la Tumbatu
25.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
26.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
27.Mhe. Haroun Ali Suleiman	Jimbo la Makunduchi
28.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
29.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
30.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
31.Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Jimbo la Chwaka
32.Mhe. Jaku Hashim Ayub	Jimbo la Muyuni
33.Mhe. Juma Duni Haji	uteuliwa na Rais
34.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
35.Mhe. Machano Othman Said	Jimbo la Chumbuni
36.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
37.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
38.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
39Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
40.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake

41.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
42.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
43.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
44.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	Kuteuliwa na Rais
45.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
46.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
47.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
45.Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
46.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
47.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	Jimbo la Dimani
49.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Jimbo la Mtoni
50.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
51.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
53.Mhe. Omar Yussuf Mzee	Kuteuliwa na Rais
54.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
55.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
57.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
59.Mhe. Said Ali Mbarouk	Jimbo la Gando
60.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
61.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
62.Mhe. Salma Moh'd Ali	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
65.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
67.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	imbo la Mwanakwerekwe
69.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
70.Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya	Kuteuliwa na Rais
71.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
72.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
73.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
74.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Jimbo la Fuoni
75.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
76.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
77.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
78.Mhe. Zahra Ali Hamad	Nafasi za Wanawake
79.Mhe. Zainab Omar Mohammed	Kuteuliwa na Rais

Kikao cha Pili - Tarehe 11 Novemba, 2010

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru sana kwa siku ya leo muhimu, kufika katika shughuli zetu za Baraza la Wawakilishi mapema. Kwa hivyo, taarifa ya leo Waheshimiwa Wajumbe ni kama ifuatavyo.

Napenda kuwapa taarifa kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein atalihutubia Baraza letu hii leo mnamo saa 4:00 za asubuhi.

Waheshimiwa Wajumbe, kifungu cha 84 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kinatamka kwamba Rais atahusika katika mamlaka ya shughuli zake, kama Rais wa Zanzibar kulihutubia Baraza la Wawakilishi wakati wowote atakaoona unafaa kufanya hivyo.

Waheshimiwa Wajumbe, tumemaliza Uchaguzi Mkuu kwa salama na amani na Mhe. Rais ameanza kuunda serikali yenye muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa mujibu wa maelekezo ya Katiba ya Zanzibar. Kwa hivyo, sasa ni fursa nzuri kwa sisi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kupata bahati hii adhimu ya kuja kuhutubiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Hivyo, Waheshimiwa Wajumbe naomba nitoe taarifa hiyo rasmi, kwamba Mhe. Rais amekubali asubuhi ya leo mnamo saa 4:00 kuja kulihutubia Baraza la Nane la Wawakilishi la Wananchi wa Zanzibar.

Kwa maana hiyo, naomba Waheshimiwa Wajumbe nyote mjitayarishe kumsikiliza pale atakapoingia, kwa ajili ya kutoa nasaha zake kwa Baraza hili la Nane leo mnamo saa 4:00 za asubuhi.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba kuwasilisha taarifa hiyo na ninakushukuruni kwa kunisikiliza.

Katibu: Mhe. Spika, suala linalofuata ni utaratibu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwa kawaida wanapokuja viongozi huwa tunawaomba waje pamoja na watu wengine ambao kwa mujibu wa Katiba ni wageni kwa Baraza hili. Hivyo, naomba nimkaribishe Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ili atoe hoja ya kuwaruhusu baadhi ya wageni ambao watafuatana na Mhe. Rais waingie ndani ya ukumbi huu na kukaa katika maeneo ambayo yamepangwa kwa ajili yao.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi atakuja kulihutubia Baraza hili leo baadaye. Vile vile kwa kuwa tumemualika Makamo wa Kwanza wa Rais ambaye yeye si Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa ajili ya kusikiliza hotuba hiyo ya Mhe. Rais.

Pia tumemualika Jaji Mkuu wa Zanzibar awe nasi katika kikao hicho. Pamoja na kwamba Mhe. Rais kwa kawaida hufuatana na mpambe wake, tunaomba Baraza likubali kuwaruhusu Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais, Mhe. Jaji Mkuu pamoja na Mpambe wa Rais waingie kwenye ukumbi wa Baraza kwa ajili hiyo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Spika: Ahsante sana, Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ndio ameanza kazi yake kama tunavyoona. Namshukuru kwa kuwasilisha hoja hiyo vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, sasa ni juu yenu kuamua baada ya hoja hiyo kutolewa, kwa hiyo wale wanaoafiki hoja hiyo kwamba Mhe. Rais aingie pamoja na wageni wetu waliotajwa wanyanyue mikono, wanaokataa, Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni kwamba mmekubali kuwa leo hii katika ukumbi wenu huu waingie pamoja na waheshimiwa wengine, ambao wametajwa na Mhe. Mwanasheria Mkuu, akiwemo Makamo wa Kwanza wa Rais, Jaji Mkuu pamoja na Mpambe wa Mhe. Rais na hawa wote watapanda katika jukwaa kuu.

Vile vile tumekubaliana kwamba ukumbi huu tumeweka alama pale nyuma, kwa maana tunayo sehemu ya wageni pale juu na pia tunayo sehemu ya wageni

maalum hapa chini. Sasa msijekustaajabu kwamba ndugu zangu Waheshimiwa Makamanda wa Vikosi mbali mbali wamo humu ndani kuna nini tena. Kwa kweli wao wamekuja kwa shughuli hii ambapo Mhe. Rais anakuja kulihutubia Baraza hili leo.

Waheshimiwa Wajumbe, tumeweka utaratibu kule nyuma kuna utepe mwekundu, ule unaashiria alama ya eneo la Waheshimiwa Wajumbe kwa maana ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi. Pamoja na hayo, katika eneo la nyuma haidhuru limo humu ndani, lakini ni eneo ambalo tumeweka kwa ajili ya wageni maalum na hasa wakati wengine wageni wanakuwa wengi na kujaa pale juu. Kwa hivyo, wale wasaidizi mbali mbali wa viongozi wako pale nyuma wamejumuika pamoja na Makamanda mbali mbali. Hali hiyo, msione ajabu kwa sababu imo katika utaratibu uliopo kwa mujibu wa Kanuni zetu.

Kwa hivyo, niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe.
Katibu kuna suala jengine?

Katibu: Mhe. Spika, kwa sasa yale ambayo tumekusudia kuyafanya yamekamilika, nadhani tuahirishe kwa ajili ya kumsubiri Mhe. Rais.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaahirisha utaratibu tunaokwenda nao mara baada ya kutoka sisi hapa, tunaomba Waheshimiwa Wajumbe mtulie humu ndani wakati tunawakaribisha Viongozi Wakuu kuja katika maeneo yetu haya, ambapo kazi ya kwanza tuliyoitayarisha kwa leo Mhe. Rais akague Gwaride Rasmi kwenye viwanja vyetu hapo nje.

Kwa hivyo, ili kuweza kufanya hivyo bila ya mtawanyiko na kupoteza muda, basi naomba sana Waheshimiwa Wajumbe mkubali, kwamba huko nitakwenda mimi kumpokea Mhe. Rais, nikifuatana na Makamo wa Pili wa Rais pamoja na Makatibu wangu hawa tutawapokea viongozi, Mhe. Rais atakagua Gwaride Rasmi na baadaye wakati ukifika tunarudi humu ndani wakati nyote mmetulia.

Kutokana na hali hiyo, mtapata nafasi ya kunong'ona pamoja na kusalimiana hapa na pale, isipokuwa kwa dharura maalum ndio tunaruhusu Mhe. Mjumbe kutoka nje. Kwa maana hiyo, tunawaomba mbakie humu ndani kwa ajili ya kubadilishana mawazo na wala mimi sijaiona hotuba ya Rais anayo mwenyewe na siwezi kuwafafanulia mna nini humo ndani. Lakini naamini yamo maneno mazuri sana ambayo anataka kutoa nasaha kwa Baraza hili.

Viongozi wetu waliombewa ruhusa na Mwanasheria Mkuu na nyinyi mkaridhia, basi watapanda huku juu pamoja na Mhe. Rais ambaye atakuwa kuliani kwangu hapa na Mpambe wake atakuwa kwenye kiti kilichotengwa

kwa ajili hiyo, wakati mkono wangu wa kushoto atakuwepo Makamo wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamadi. *(Makofi)*

Ahsante sana. Vile vile Jaji Mkuu wa Zanzibar Mhe. Hamid Mahmoud Hamid naye atakuwa kushoto baada ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwenye viti vilivyopangwa kwa ajili yao.

Wasaidi wa waheshimiwa hawa tukiachia Mpambe wa Rais wote watakuwa kwenye mstari wa nyuma, ili wakati wowote wanapohitajika waweze kutoa huduma inayohitajika.

Waheshimiwa Wajumbe, ninakushukuruni kwa kunisikiliza kwa utaratibu huo tulioweka. Nadhani muda unaweza kuwa mrefu kidogo, kwa sababu hivi sasa tunazo kama dakika 45 kufikia saa 4:00, lakini nafikiri mtaweza kuvumilia kwa muda huo, kwa ajili ya kumsubiri Mhe. Rais.

Kwa kuwa nimeona mkono wa Mhe. Haji Faki Shaali, basi ni vyema nimruhusu labda anahitaji kuuliza au kusema chochote.

Mhe. Haji Faki Shaali: Nakushukuru Mhe. Spika. Pamoja na kumaliza kazi yangu ya Unadhimu kwa heshima katika kipindi kilichopita. Lakini kwa heshima ya chama changu bado napenda kusema kwamba gazeti la jana la Zanzibar Leo kwa bahati mbaya na wala hawakukusudia wamepotosha kidogo majina ya waheshimiwa ambao walituandika.

Kwa mfano, kuna Mhe. Abdalla Juma Abdalla wa Jimbo la Chonga, badala yake wamemuandika Mhe. Omar Khamis Juma ambaye huyu alikuwa mgombea wa CCM na wala hakubahatika. *(Kicheko/Makofi)*

Pili Mhe. Spika, kuna Mhe. Mohmmed Mbwana Hamadi wa Jimbo la Chambani jina lake kwa bahati mbaya ameandikwa mwanamke Bahati Khamis Kombo, pia huyu alikuwa ni mgombea wa Chama cha CCM ambaye hakubahatika. *(Kicheko/Makofi)*

Vile vile kuna Mhe. Omar Ali Shehe naye jina lake ameandikwa Suleiman Farahani Said ambaye alikuwa mgombea wa CCM na wala hakubahatika. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, nayazungumza haya, ili ndugu zetu wa vyombo vya ulinzi na usalama wasije wakawasumbua hawa katika maeneo ya kusafiria kama vile *Airport* na bandarini wakambiwa wewe siye.

Nakushukuru Mhe. Spika. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika: Namshukuru sana Mhe. Haji Faki Shaali. Kwa kweli vitu hivi *referee* tu Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Kwa kweli tume imetuletea majina ya waheshimiwa mbali mbali waliofanikiwa kuchaguliwa kwenye majimbo yao, waliopita kwenye Viti Maalum pia na wale walioteuliwa na Mhe. Rais ikiwa pamoja na Mwanasheria Mkuu wetu wa Zanzibar, wameletwa rasmi kwa majina yao.

Hivi sasa Waziri wa Habari bado hatuna ambaye angeomba radhi na baadaye kusema anarekebisha. Kwa hivyo, mimi kwa niaba ya serikali na idara ambayo inahusika na utoaji wa gazeti hilo, naomba radhi sana na ninawaamuru wahariri wa gazeti hilo kesho wafanye marekebisho na yaonekana kwenye ukurasa wa mbele kwa yale yote yaliyokosewa, ili yaendane na ile taarifa rasmi iliyotolewa na Tume ya Uchaguzi. Vile vile nimuombe mhariri huyo aje afisini na kupewa majina sahihi hasa kwa yale yaliyokosewa.

Kwa niaba yao waheshimiwa wajumbe ninakuombeni radhi sana na hilo ni kosa au bahati mbaya. Hivyo, nawaomba radhi sana wale wote waliodhulumiwa maana hiyo ni dhulma, bila ya shaka imewauma kwa kiasi fulani. Kwa mfano, Mhe. Abdalla Juma Abdalla wa Jimbo la Chonga naamini imemuuma sana, kwa sababu aliniuliza hapo nje baada ya kuona gazeti hili aingie au vipi, nilimwambia aingie. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri tunamwiwiya radhi kwa radhi niyoomba kwa niaba yenu kwa makosa yaliyotendeka. Nakushukuruni sana.

Kwa hivyo, baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe naahirisha kikao hiki kwa muda kwa ajili ya kumsubiri Mhe. Rais wa Zanzibar aje na tumpokee, akague Gwaride la Heshima na baadaye arudi humu ndani. Nadhani makamanda wao wanaweza kuwa kwenye gwaride kuona askari wenzao wanafanya nini.

Nakushukuruni sana.

(Saa 3:20 asubuhi Baraza liliahirishwa mpaka saa 4:00 asubuhi)

(Saa 4:08 asubuhi Baraza lilirudia)

Katibu: Hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika: Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Moh'd Shein, Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad, Mhe. Jaji Mkuu wa Zanzibar Hamid Mahmoud Hamid.

Waheshimiwa Wajumbe nilitoa taarifa mapema asubuhi kwamba leo tutakuwa na ujio wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambaye hivi sasa yuko tayari ameshafika katika ukumbi wetu huu. Namshukuru sana Mhe. Rais pamoja na Makamo wa Rais na Mhe. Jaji Mkuu kupata wasaa wa kuja kwenye shughuli yetu ya Baraza, ili Mhe. Rais apate nafasi ya kulihutubia rasmi Baraza hili leo hii tarehe 11 saa hizi tulizonazo.

Tayari Mhe. Rais ameshakagua gwaride la heshima hapo nje kama vile nilivyowaarifu mapema, sasa kazi iliyobaki ni kumsikiliza yeye ili aweze kutoa hotuba.

Lakini Mhe. Rais na Waheshimiwa Wajumbe kabla sijafanya hivyo, naona ukumbi wangu pale juu umejaa wageni mbali mbali tuliowaalika. Ningependa basi niwatambue wale wageni mbali mbali tuliowaalika na nitawaomba sana wale nitakaowataja basi anyanyuke kitini alipo, anaweza akapunga mikono kidogo na Waheshimiwa Wajumbe mnaweza mkaangalia kwa nyuma kidogo, ili mkamtazama huyo mgeni wetu aliyepo pale juu kwenye ukumbi wa wageni wa Spika.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe kati ya wageni tuliowaalika kwenye shughuli yetu ya leo ya kusikiliza hotuba ya Mhe. Rais ni Mhe. Mama Mwanamwema Shein, yule pale. *(Makofi)*

Wake wa viongozi wako wengi. Mwengine ambaye anashiriki kwenye shughuli hii muhimu ya leo ni Mhe. Mama Asha Seif Ali Iddi. *(Makofi)*

Lakini leo hii ni siku maalum, kati ya viongozi na mwenzenu Pandu Ameir Kificho yumo. Kwa hiyo, nae amefuatana na wake zake. Hao ni Mhe. Aziza Kificho namuomba anyanyuke na Mhe. Neema Kificho. Waheshimiwa Wajumbe niwaombe radhi wa tatu ana dharura. *(Kicheko/Makofi)*

Nakushukuruni sana kwa makofi hayo. Wengine kati ya wageni wetu mashuhuri waliofika hapa ni Mhe. Waziri Kiongozi Mstaafu, Mhe. Ramadhan Haji Faki, yule pale. *(Makofi)*

Katika shughuli hii tumewaalika vile vile waheshimiwa mabalozi wadogo waliopo nchini hapa pamoja na mabalozi wengine wote. *So could I call all His Excellencies to stand up to be seen by the members,* wale pale. *Thank you so much indeed.*

Lakini katika shughuli hii muhimu tumewaalika na viongozi mbali mbali wa vyama vya siasa, walioko hapa juu nawaomba wao wasisimame kwa sababu

wao tayari wanaonekana hapa. Lakini wale wageni wetu tuliowaalika pale juu viongozi mbali mbali wa vyama vya siasa nawaomba kwa pamoja wasimame. *(Makofi)*

Nakushukuruni sana.

Waheshimiwa Wajumbe, mtakubaliana na mimi kwamba ukumbi huu ambao tumo umejengwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwa mashirikiano makubwa sana na ndugu yetu Sheikh Abdalla Mohammed ALLYOUSEIF na yeye yupo pale. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naomba nikupeni taarifa kwamba kwa msaada mkubwa aliyotupa mzee huyu kuna ukumbi mwengine pale juu wa mikutano utaitwa kwa jina la Sheikh Mohammed Abdalla ALLYOUSEIF. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana hatuwezi kuwamaliza wote. Lakini nikuombeni sana kwamba karibuni na mniwiye radhi kwa kuwa sikuweza kuwataja wote, kwa hiyo karibuni sana katika shughuli yetu hii muhimu ya kusikiliza Hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Vile vile kwenye ukumbi wetu mdogo hapa chini tunao Makamanda, naomba makamanda wale mbali mbali wa Vikosi vya (SMZ) pamoja na makamanda wa Polisi na Jeshi pale walipo wasimame ili nao waonekane na wananchi. Asanteni sana. (*Makofi*).

Waheshimiwa Wajumbe mtakubalina na mimi kwamba makofi haya mnayoyapiga humu ndani kwa furaha zote yamekuja baada ya kazi nzuri sana iliyokwenda kwa amani na utulivu baada ya uchaguzi mkuu uliofanyika tarehe 31, Oktoba mwaka 2010. Kazi hiyo imefanywa sio na mwengine isipokuwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar. Namuomba asimame. (*Makofi*).

Nawaomba basi Makamishna wa Tume na Mkurugenzi kama wapo pia nao wasimame ili nao waonekane waliofanya kazi nzuri ya uchaguzi mkuu kama wapo.

Waheshimiwa Wajumbe nafikiri kwa kuwa tayari nimewataja wageni mbali mbali wale wangine ambao sikuwataja naomba radhi sana. Haikuwa rahisi kuweza kuwataja wote. Lakini wote nawakaribisha katika ukumbi wetu huu ili kusikiliza hotuba ya Mhe. Raisi.

Wakati tunajitayarisha kusubiri hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar, labda niombe nitoe taarifa ndogo tu.

Mara baada ya shughuli hii ya hotuba ya Mhe. Rais tutakuwa na picha ya pamoja hapo nje, ambayo itakwenda kwa utaratibu wa viongozi tuliokuwepo hapa meza kuu, tukijumuika pamoja na Mhe. Makamo wa pili wa Rais na Mhe. Mwanasheria Mkuu pamoja na Katibu wangu pamoja na Waheshimiwa Wajumbe. Wajumbe wataingia kwa makundi ya wajumbe ishirini ishirini mpaka tuwamalize. Baadaye picha nyengine zitakuwa zinaendelea za watumishi wetu wa Bara. Baadhi ya viongozi wageni mashuhuri waliopo pale juu ambao tumewataja hapa watakuwa wameshiriki katika picha hiyo.

Tutapotoka hapa tutatoka kwa utaratibu kama tulivyokuja. Mimi na Mhe. Rais tutapita upande wa kulia wangu. Waheshimiwa Makamo wa Kwanza wa Rais pamoja na Mhe. Jaji Mkuu watatoka kwa upande wa mkono wa kushoto wangu. Tutajipanga kama tulivyokuja. Nitawaomba waheshimiwa wajumbe nyinyi mtulie ili tutoke halafu tena na nyinyi mtatoka kwa utaratibu. Mhe. Makamo wa pili wa Rais baadaye tutajumuika naye wakati tukipumzika kidogo tukisubiri utaratibu wa upigaji picha.

Mhe. Rais sasa wakati umefika wajumbe hawa ambao wapo kwa utulivu wana hamu kubwa kukusikiliza Mhe. Rais ili utoe nasaha zako. Lakini vile vile wageni waalikwa wengine mara baada ya kuapishwa pale uwanja wa Amani hawakupata kuwa karibu na wewe walikuwa kwenye majukuu ya mbali. Leo wameona waje wakusikilize na wakuone kwa karibu zaidi katika ukumbi huu kwa hivyo nao wapo tayari kabisa kutaka kusikia neno lako la hekma ambalo utatuelekeza katika Baraza letu hili.

Mhe. Rais sasa nikuombe uelekee kwenye sehemu yetu ili ulihutubie Baraza. Mhe. Rais karibu sana. (*Makofi*).

HOTUBA YA MHE. RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI, DK. ALI MOHAMMED SHEIN KATIKA UZINDUZI WA BARAZA LA NANE LA WAWAKILISHI TAREHE 11 NOVEMBA, 2010

Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar,
Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais,
Mhe. Makamo wa Pili wa Rais,
Mhe. Jaji Mkuu wa Zanzibar,
Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar,
Waheshimiwa Mabalozi wadogo mliopo Zanzibar,
Wawakilishi wa Mashirika mbali mbali ya Kimataifa,
Waheshimiwa viongozi wa vyama vya siasa,
Ndugu wageni waalikwa, mabibi na mabwana, Assalaama Aleykum.

Namshukuru Mwenyezi Mungu, Mola wetu mwenye wingi wa Hekma, Muumba Mbingu na Ardhi na vyote viliomo ndani yake, kwa kutupa Rehema yake na uzima pamoja na uwezo wa kukutana hapa leo katika ghafla hii adhimu na muhimu kwa nchi yetu. Namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie mafanikio makubwa katika azma yetu hii ya uzinduzi wa Baraza la Wawakilishi la Nane la Zanzibar nakupeni hekma na busara Waheshimiwa Wajumbe wote ili muweze kutekeleza majukumu yenu ya Kikatiba na ya Kisheria kwa mafanikio makubwa katika kuendeleza nchi yetu na kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Zanzibar.

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu shukurani zangu za dhati nazielekeza kwa wananchi wote wa Zanzibar kwa kushiriki kwao Kikamilifu katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 31, mwaka huu na kutuwezesha kuwapata Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Shukurani zangu maalum kwa wananchi na viongozi mbali mbali wa vyama vya siasa, vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na Tume ya Uchaguzi kwa kuwezesha mchakato mzima wa uchaguzi kufanyika kwa njia ya amani, usalama na utulivu mkubwa.
Tumeweza kushindana bila ya kukashifiana na bila ya kugombana. Tumeuonesha ulimwengu kwamba Wazanzibari wakiamua wanaweza. (*Makofi*).

Tunao uwezo wa kutumia haki na demokrasia yetu ya kuchagua na kuendelea kubaki tukiwa na umoja wetu. Tujipongezini sana na tujipe hongera sote wananchi wa Zanzibar. Mwenendo wa wananchi katika mchakato mzima wa uchaguzi tokea wa uwandikishaji wa upigaji kura hadi kutolewa matokeo kumeipatia sifa kubwa nchi yetu na taifa letu la Tanzania kwa ujumla duniani kote.

Hivi karibuni nimeonana na baadhi ya viongozi wa Jumuia ya Afrika na wengine na wametoa sifa kubwa sana kwa jitihada zetu za kufanikisha uchaguzi wa haki na huru na usalama nchi kwetu.

Ni vyema kukumbuka kwamba hali hiyo imechangiwa zaidi na maridhiano mema ya vyama vyetu vikuu vya siasa yaani Chama cha Mapinduzi na Chama cha CUF. Leo ni mwaka mmoja na wiki moja tangu pale ule mkutano wa kihistoria baina ya Rais wa Zanzibar Mstaafuu na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Amani Abeid Karume na Katibu Mkuu wa CUF, Maalim Seif Sharif Hamad kukutana.

Mkutano huo ulifanyika Ikulu ya Zanzibar November tano mwaka 2009 umebadilisha hali ya kisiasa na hali ya kijamii ya Zanzibar na kufungua sura mpya ya ushirikiano, umojia, amani na utulivu. Kadhalika hatua hiyo ilifuatiwa na kura ya maoni ambapo wananchi walio wengi walitoa ridhaa yao kwa asilimia 66.4 kwa mfumo mpya wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Zanzibar.

Baraza la Wawakilishi nalo lilifanya marekebisho ya 10 ya Katiba yetu yaliyopelekea kuanzishwa kwa mfumo huo mpya wa Serikali. Nalishukuru kwa dhati kabisa na nalipongeza sana Baraza lililopita kwa kupitisha marekebisho hayo yaliyosaidia kwa kiwango kikubwa sana katika kudumisha utulivu wa nchi yetu. Ahsante sana Waheshimiwa Wawakilishi.

Tunakutana leo hapa katika hali na sura ya amani. Naamini ndio itakuwa inatupa muongozo katika utekelezaji wa shughuli za Baraza hili katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Hatuna budi kutoa shukurani zetu nyingi kwa Mhe. Rais Mstaafu Dk. Amani Abeid Karume, kwa busara zake na hekma zake zilizopelekea kufikiwa kwa maridhiano hayo pamoja na ndugu yetu Mhe. Seif Sharif Hamad.

Kwa hakika tunawapongeza kwa ujasiri wao mkubwa. Aidha nawashukuru wananchi wote wa Zanzibar kwa kuukubali mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kupitia kura ya maoni iliyofanyika tarehe 31/7/2010. Nawapongeza sana wananchi wa Zanzibar na nawambia ahsante sana.

Ndani ya mfumo mpya kwa mara ya kwanza tutaunda Serikali ya Ummoja ya Kitaifa yenye kuvishirikisha vyama vyetu viwili vikuu ambavyo ndivyo vilivyochaguliwa na wananchi wa Zanzibar kuwakilisha katika Baraza hili tukufu. Napenda pia kumshukuru sana Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuiyunga mkono Zanzibar na viongozi wake katika mchakato mzima wa kuleta maridhiyano. Wakati huo huo kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar nampongeza kwa ushindi wake wa kishindo katika uchaguzi Mkuu wa Uraisi wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania. Nampa hongera kubwa sana Mhe. Dk. Kikwete. Napenda nimuahidi kwamba ushirikiano wa karibu baina ya mimi na yeye na Serikali zetu mbili utaendelea kufanikiwa sana katika kipindi hichi tulichonacho.

Shukurani zangu nyengine nazielekeza katika Chama changu Chama cha Mapinduzi kwa kuniteuwa na kuniunga mkono ili niweze kuwakilisha katika mchakato wa kugombania ridhaa ya wananchi kupitia ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2010 na hatimaye kupata ushindi wa kuiyongoza Zanzibar. Naishukuru CCM na viongozi wake wote kwa kunipa heshima hiyo na kuniwezesha kulibeba jukumu hilo zito kwanza hili la kampeni na kunadi sera zetu kupitia ilani ya uchaguzi ya chama chetu, ilani ya mwaka 2010/2015.

Kazi kubwa na mpangilio mzuri wa Kampeni za uchaguzi huo ndio uliowavutia wanachama na wananchi mbali mbali wa Zanzibar na kuziunga mkono sera zetu na hivyo kuipa ridhaa CCM na viongozi wake ya kuendeleza kuiyongoza nchi yetu na Serikali yake kwa kipindi kingine cha miaka mitano.

Serikali yangu ya awamu ya saba chini utaratibu wa Katika ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa itasimamia kwa dhati kabisa utekelezaji wa ilani yake na kudumisha amani, utulivu na umoja wa Wazanzibari wote kwa kushirikiana na wahusika wote wenye hamu na maendeleo ya nchi yetu. Ishallah kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu tutafanikiwa.

Lakini vile vile natoa shukurani zangu maalum kwa wananchi wa Zanzibar kwa kukichagua Chama cha Mapinduzi. Nimepokea matokeo ya uchaguzi kwa heshima kubwa. Navishukuru vyama vyote vyengine vya siasa vilivyoshiriki katika uchagu mkuu na kutoa ushindani mkubwa kwa CCM, nawapongeza kwa kutumia haki yao hiyo ya kidemokrasia kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibara ya mwaka 1984.

Shukurani za dhati kabisa nazitoa kwa Chama cha CUF nacho kwa kushiriki katika uchaguzi mkuu ulioendeshwa kwa amani na utulivu na ambao ulikuwa huru na wa haki. Kwa sasa uchaguzi mkuu umekwisha na sote tumeshikamana katika kuunda Serikali ya Umoja ya Kitaifa ya Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi ya awamu wa saba itaongozwa na utaratibu mpya wa umoja wa kitaifa.

Ni jukumu letu kuzidisha ushirikiano na utulivu ili kuelekeza nguvu zetu sote katika kuwaletea wananchi waliotuchagua maendeleo wanayotegemea. Aidha napenda kukushukuruni nyote Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kukubali kujitokeza kugombea ujumbe wa Baraza la Wawakilishi, kupitia mchakato mgumu na mrefu tangu kuchukua fomu kenye vyama vyenu vya siasa, kupitia mchakato wa kura za maoni, kufanya kampeni hadi kutangazwa kuwa nyinyi ni washindi wa majimbo mliochaguliwa.

Naamini kwa dhati katika nafsi yangu kwamba mtawawakilisha wananchi waliokuchaguweni kwa haki na uhuru na kwa mustakbali wa majimbo hayo na mustakbali wa Zanzibar. Naamini kwamba mtafanya kila linalostahiki kwa mujibu wa katiba na kanuni za Baraza la Wawakilishi ili kuwawakilisha wananchi kwa kushirikiana na serikali yao. Katika kuwahudumia wananchi wote wa Zanzibar bila ya kujali itikadi zao za kisiasa, dini au jinsia. Naamini kwamba mtatumia fursa hii kutoa maoni yenu mbali mbali yenye shabaha ya kuleta ufanisi, kuongeza kasi ya maendeleo na kuongeza ustawi katika nchi yetu. Nakuombeni utumishi wa mafanikio na mashirikiano makubwa katika miaka mitano ijayo ndani ya Baraza letu hili tukufu.

Mhe. Spika, kwa dhati kabisa napenda nichukue nafasi hii kukupongeza wewe Mhe. Pandu Ameir Kificho kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Spika, wa Baraza la Nane la Wawakilishi la Zanzibar. (*Makofi*).

Naamini kwamba Waheshimiwa Wajumbe wanakukubali na wanakuamini na ndio maana wakaamua kukukabidhi jukumu hilo zito la kuliongoza Baraza hili. Ninahakika aamini kwamba una uwezo mkubwa wa kuliendeleza Baraza hili. Una elimu na ujuzi wa kutosha kuliongoza Baraza letu kwa busara zaidi na kwa hekma kubwa na uwadilifu kama ilivyokawaida yako katika mabaraza yaliyopita. Hongera sana Mhe. Spika. Sina shaka na naamini ndani ya nafsi yangu kwamba wajumbe watakupa ushirikiano wa kutosha katika kukiendesha chombo hiki kikubwa na muhimu.

Mhe. Spika, tofauti na mabara saba yaliyopita, Baraza hili la nani ni la aina yake pekee, ambapo kuna mabadiliko yaliyotofauti na mabaraza saba yaliyopita.

1) Zaidi ya nusu ya wajumbe wa Baraza hili ni wapya. Kwa maana ya kwamba idadi kubwa ya wajumbe hao ni mara yao ya kwanza kuingia kwenye chombo hiki cha kutunga sheria.

2) Idadi ya waheshimiwa wajumbe wanawake imeongezeka kiasi cha kutia moyo na matumaini makubwa ya Baraza letu.

3) Idadi ya waheshimiwa wajumbe wenye umri mdogo yaani vijana imeongezeka sana Baraza hili na nane.

4) Baraza hili litakuwa ni la kwanza na la kihistoria kwa Zanzibar kwa kusimamia Serikali mpya ya Umoja wa Kitaifa kwa hivyo kukabiliwa na changamoto ya kufanya kazi katika mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Lakini ndani ya msingi wa kushirikiana kwa pamoja kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Naamini jukumu hilo Waheshimiwa Wajumbe mtalitekeleza kwa ufanisi mkubwa na kuwaridhisha ndugu zetu Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, tunaianza awamu hii ya nane ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tukiwa tumebeba dhima na matumaini makubwa ya Wazanzibari. Kwa vile tumekubali kuwatumikia vyema wananchi wenzetu na kuwatatulia shida zao mbali mbali. Ni lazima tuelewe vyema dhima tuliyoibeba pamoja na kuzifahamu shida zao mbali mbali. Katika utekelezaji wa hayo hatuna budi kujue tulipo hivi sasa na kadhalika tujue tunapokusudia kwenda. Tukiyatambua hayo tutakuwa tumeifahamu vyema dhima yetu kwa wananchi waliotuchagua. Kwa vile tumekubali kuwatumikia kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Mhe. Spika, ni matumaini ya wananchi wetu wote wa Zanzibar kwamba tutaendeleza mambo yote ya maendeleo yaliyofanywa katika awamu zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa kufanya hivyo tutaweza kutekeleza kwa kiasi kikubwa mageuzi yote yaliyoanzishwa, sera zilizopitishwa na sheria zilizotungwa ili zisimamie uimarishaji wa uchumi na huduma za jamii na hivyo kuwapunguzia ukali wa maisha wananchi wote bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

Kama tunavyofahamu kutokana na utafiti wa mapato wa matumizi ya kaya iliyofanyika mwaka 2004/2005 watu 49 katika kila watu 100 wamo katika umasikini wa kipato. Hivyo Serikali kupitia MKUZA itachukua hatua mbali mbali za kuwapunguzia wananchi umasikini wa maisha na makali yake. Kuimarika kwa maisha ya wanachi wa Zanzibar kuna maanisha ungezeko la vipato vyao kwa mujibu wa shughuli zao zilizohalali wanazozifanya. Hali hii inatokana kuongezeka kwa fursa za ajira na kujiajiri katika sekta iliyo rasmi na ile isiyo rasmi.

Ni muhimu kuyajenga na kuyaimarisha mazingira ya biashara, mazingira ya uzalishaji wa mali na huduma za kuwafikisha karibuu zaidi na huduma za nishati, maji, usafiri, masuala ya uchukuzi na mawasiliano. Vile vile kupatikana kwa mahitaji na mitaji kwa wepesi na taarifa juu ya masoko ya bidhaa na huduma zilizozalishwa.

Misingi ya huduma huu imo kwenye ilani ya uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010. Katika utekelezaji wa ilani hii program za sekta mbali mbali zitaangalia ili kukidhi utekelezaji wake na kuzifikisha huduma mbali mbali katika maeneo yote karibu na wananchi ili kuinua hali zao za maisha.

Mhe. Spika, wananchi wanatarajia kutokana na mazingira hayo waweze kukidhi mahitaji yao ya lazima ya chakula tena chenye lishe nzuri, mavazi, makaazi ya kuridhisha, wapate elimu, huduma za afya, huduma za maji safi la salama kwa wao na vizazi vijavyo kwa uhakika zaidi. Ni matarajio yao pia kwamba jitihada hizi zitapelekea kupungua kwa kasi ya maambukizi ya virusi vya Ukimwi, matumizi ya madawa ya kulevya. Kwa lengo la kuinusuru jamii na hasa vijana.

Tunatarajia usawa, wajibu na fursa baina ya wanawake na wanaume zitaongezeka. Kadhalika matumaini yao pia ajiwa kwa watoto wadogo na udhalilishaji unapigwa vita kwa nguvu zote.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili matumaini haya ya wananchi ni makubwa. Lakini kubwa zaidi ni matumaini ya jinsi ya kuyafikia wananchi wanatarajia na watafaidika zaidi ikiwa hawatabakia kama waangalizi tu katika harakati za kuwafikia matarajio yao. Naamini watafarijika zaidi iwapo na wao wenyewe watakuwa ni washiriki watendaji katika ufanyaji wa maamuzi na utekelezaji wa mambo ambayo tutakuwa tumeyaamua kwa pamoja. Kwa njia hiyo basi wananchi wenyewe watayamiliki na kuyaongoza mabadiliko yatakayokuwa yanatokea na hivyo kuweza kuyatunza na kuyadumisha.

Wananchi wanahitaji utekelezaji wa demokrasia kwa vitendo. Hili litawezekana pale tutakapoweza kuziimarisha serikali zetu za mitaa, jumuia za kiraia na jumuia za wananchi, hii ni dhima kubwa kwetu. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya awamu ya saba itahakikisha kwamba itatekeleza suala hilo kama lilivyofafanuliwa katika sera na Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 kwa kuwashirikisha wote pamoja na makundi ya mahitaji maalum.

Fursa hizi za ushiriki hazina budi ziwe na muunda mpana zaidi, unahusisha makundi mbali mbali ndani ya jamii, Wanawake, vijana na makundi yenye mahitaji maalum yote, hayana budi ya kupata fursa za kushiriki katika maamuzi na utekelezaji wa maamuzi hayo kwa manufaa ya wote. Ni jambo la faraja kwamba juhudi zetu hazitakuwa zinaanzia mbali. Awamu mbali mbali za uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilizotangulia tayari zimetandika misingi madhubuti ya mambo hayo. Miundo mbinu imara ya barabara imetandikwa nchi nzima Unguja na Pemba, mijini na vijijini. Nishati ya umeme hivi sasa imefika maeneo mengi sana ya Unguja na Pemba kwa karibu asilimia 75.

Upatikanaji wa maji safi na salama umefikia asilimia 60 kwa mijini na 60 kwa vijijini. Changamoto yetu ni kuhakikisha kwamba tunakamilisha kwa asilimia

100. Na kwa juhudi ya kuimarisha mabomba ya usambazaji maji ili maji yawe karibu zaidi na makaazi ya wananchi.

Huduma za mawasiliano kwa njia ya simu za mikonono na mitandao ya Intenent inapatikana kila pembe ya nchi yetu Unguja na Pemba. Misingi ya amani, utulivu na umoja miongoni mwa wananchi inaendelezwa sana katika uongozi wa awamu ya sita ya Mhe. Dk. Amani Abeid Karume. Kazi inayotusubiri hivi sasa ni kuziimarisha huduma hizi za kiuchumi na kijamii ili wananchi waweze kuzitumia kwa manufaa ya kuinua ubora wa maisha yao.

Kwa kulinganisha nchi nyengine za Afrika ni kwa kuzingatia malengo ya melenium ndani ya chaguzi wa CCM zilizopita Zanzibar zilifikia hatua ya kupigiwa mfano katika mambo mengi sana ikiwa ni pamoja na mitandao ya miundo mbinu, mawasiliano, huduma za elimu na afya, jitihada za kupambana kwa kuenea virusi vya Ukimwi, mapambano dhidi ya maleria, upatikanaji wa maji safi na salama, umeme na ustawi wa jamii kwa jumla. Niwajibu wetu hivi sasa kuyalinda mafanikio haya na kuyaendeleza ili tuweze kufikia viwango vya juu zaidi vya kimataifa. Hii ni kazi iliyombele yetu.

Mhe. Spika, nilipokuwa katika kampeni za uchaguzi wa Urais niliwaeleza wananchi ahadi mbali mbali kwa mujibu wa ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi, ilani ya mwaka 2010 na 2015.

Napenda kutamka wazi kwamba utekelezaji wa ahadi hizo katika ilani utakuwa ndio msingi wa mwelekeo mkubwa wa serikali inayoongoza programu mbali mbali za utekelezaji wa ilani hizo zitatayarishwa na kila wizara. Matarajio yangu ni kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili watashirikiana kikamilifu katika kuiwezesha serikali yetu, ili ifanikiwa katika malengo hayo.

Tumeingia katika Mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na hii ina maana itakuwa ni serikali yenye kujali maslahi ya wananchi wote na matakwa yao. Naamini kwamba tutatekeleza wajibu wetu kufuatana na Mapinduzi matukufu ya Januari 12, 1964 ya kuleta umoja, mshakamano na mapenzi baina yetu, ambapo ni wajibu wetu sote kuyaenzi, kuyathamini Mapinduzi kwa kufanyakazi kwa pamoja kwa bidii zaidi na kwa manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Spika, serikali yangu ninayoiongoza itatoa kipaumbele katika sekta mbali mbali. Nachukua fursa hii kueleza baadhi ya madhumuni yake kama nilivyokwisha kuyaeleza hayo wakati ambapo nilikuwa nikiomba kura kwa wananchi wa Zanzibar. Maeneo makubwa katika hayo yatakuwa ni ukuaji wa uchumi wetu, ustawi wa huduma za jamii, uimarishaji wa miundombinu, sekta za uzalishaji, maadili ya viongozi na watumishi, utawala bora, utumishi na wafanyakazi, umoja wa wananchi na udumishaji wa Muungano wetu.

Mhe. Spika, ni ukweli usiopingika kwamba miongoni mwa vigezo ambavyo wananchi walivyovutiwa navyo na kuipeleka CCM kuongeza tena Zanzibar, ni mafanikio makubwa ya utekelezaji wailani yetu ya uchaguzi wa mwaka 2005 yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Dk. Aman Abeid Karume.

Lakini pamoja na utekelezaji huo wa mafanikio bado tuna changamoto kadhaa katika kujiletea maendeleo yetu. Serikali ya Mapinduzi ya Awamu ya Saba jukumu lake la kwanza katika kushughulikia suala la uchumi, ni kuendeleza mafanikio yote yaliyofanywa katika kipindi kilichopita hadi sasa. Kama nilivyoeleza katika ilani yetu, tumedhamiria kuitoa nchi yetu katika uchumi tegemezi kwenda kwenye uchumi wa kisasa, na hivyo katika kufanikisha azma hiyo tutatoa vipaumbele katika matumizi ya maarifa ya kisasa ya sayansi na teknolojia.

Tutawaandaa wananchi wetu kimaarifa na kimwelekeo, tutafanya mapinduzi ya kilimo, mapinduzi ya biashara na viwanda, mapinduzi ya uvuvi. Ambavyo ndivyo kiongozi wa uchumi wa kisasa na kufanya mapinduzi katika nishati na miundombinu. Lengo hapa likiwa ni kuchochea uwezo wa kuongeza uzalishaji ambao itawezekana kutokana na kuongezeka kwa ufanisi na tija za ziada katika uchumi wetu. Hivyo basi majukumu ya msingi ya serikali yangu yatakuwa ni kuimarisha na kuboresha elimu, kuandaa rasilimali watu katika maarifa na mwelekeo.

Halikadhalika serikali yangu itainua matumizi ya maarifa ya sayansi na teknolojia na kuhakikisha kwamba Serikali ya Awamu ya Saba inatia mkazo mkubwa na kutoa kipaumbele katika uendelezaji wa utafiti, kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, serikali ya awamu saba itatumia kikamilifu huduma za utafiti kwa kushirikiana na kamisheni ya sayansi na teknolojia ya Tanzania. Kila taasisi iliyomuhimu itawajibika kuwa na kitengo cha utafiti kwa ajili ya maendeleo ya sekta yake. Ni jambo la kupongeza sana kwamba ziko sekta. Mfano, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Kilimo Mazingira na Misitu, tayari zimepiga hatua kubwa katika utafiti na mambo mbali mbali.

Aidha, sekta nyengine nazo zitaimarishwa na kuagizwa zishughulikie sana upande wa utafiti, kwani maendeleo hayapatikani bila ya kufanya utafiti kwa kutumia sayansi na teknolojia.

Vile vile vyuo vikuu vya Zanzibar vitashajihishwa ili viendeleze utamaduni wa kufanya utafiti katika kazi zake za kila siku, ili wafanyakazi na wahitimu wake wawe na uwezo wa kufanya utafiti katika masuala mbali mbali ya kijamii, ya

kiuchumi na kadhalika. Wakati huo huo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba, itaongeza upatikanaji wa nishaati yenye uhakika na nishati mbadala pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kisasa.

Tutaendeleza usimamizi wa sera za sheria na uwekezaji ili kuchochea kasi ya uwekezaji na ujenzi ya misingi ya uchumi endelevu unakua na kuendeshwa na nguvu za soko, huku tukilenga kuwawezesha wananchi kiuchumi na uchumi wetu tunaulenga ukuwe kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2005 na kupunguza kiwango cha mfumuko wa bei hadi chini ya asilimia 7 na kuongeza kipacho cha kila Mzanzibari, kutoka kiwango cha sasa cha Shs. 726,000/= kwa mwaka hadi kufikia kiwango cha Shs. 880,000/= ifikapo mwaka 2015.

Tutaimarisha udhibiti na mapato ya matumizi ya serikali na kuziba mianya yote ya uvujaji wa mapato ya serikali. Tutahakikisha kwamba viwango vya ukusanyaji wa mapato ya ndani tunaviimarisha na kuviongeza. Katika eneo hili tutajipanga kusimamia utekelezaji wa sheria za fedha, zikiwemo kodi za makampuni na kuimarisha miundombinu ya kiuchumi.

Mhe. Spika, mwelekeo wa mageuzi katika hali ya uchumi wetu utategemea sana ushirikiano baina ya vyombo vya umma na taasisi binafsi. Serikali itaimarisha ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi kwa msingi wa *public private partnership* au njia nyengine.

Mafanikio katika programu hii ya mageuzi yanatarajiwa yapelekee ongezeko la ukuaji wa uchumi kutoka ukuaji wa sasa wa asilimia 6.7 mwaka 2009 hadi kufikia asilimia 10 kama nilivyosema mwanzo mwaka 2015.

Mhe. Spika, muundo wa uchumi wetu utajikita zaidi katika maendeleo ya sekta ya utalii, viwanda vidogo vidogo na viwanda vya kati na sekta ya kilimo. Shughuli za utalii kama sekta kiongozi zitazidi kuimarishwa na kufungua soko lake kwa wazalishaji na watoa huduma za ndani na wazalendo watajengewa uwezo zaidi ili wawezeshe kuzalisha bidhaa na huduma zinazokidhi haja na viwango vya soko letu la utalii.

Kwa msingi huo, utalii utasaidia sana katika kukuza ajira na kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2020 asilimia 50 ya watu wote wenye uwezo wa kufanya kazi wanaajiriwa ndani ya sekta ya utalii.

Pamoja na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na mpango mkuu wa utalii, sekta hiyo itafanyakazi ya kuwa ni kichocheo cha maendeleo ya sekta ya viwanda vidogo vidogo, viwanda vya kati, sekta ya kilimo hasa cha mboga mboga na matunda, ufugaji, mapinduzi ya uvuvi, ambazo zitakuwa zinazalisha bidhaa kwa ajili ya sekta ya utalii.

Pia utalii utakuwa ni kichocheo cha maendeleo ya sekta ya biashara, usafirishaji na uchukuzi wa barabara, bahari na anga. Hii ndio sura ya sekta ya utalii tunayoitarajia kama sekta kiongozi. Msisitizo huu utabainishwa kwa uwazi zaidi ndani ya sera ya mpango mkuu na mpango wa maendeleo ya sekta ya utalii. Serikali itasisitiza kujengeka kwa utalii wenye kuheshimu mila zetu, wenye kuheshimu desturi zetu na utamaduni wa Mzanzibari.

Utalii wa Zanzibar utaimarishwa ukiwa na misingi endelevu, yenye kuendeleza na kuyachunga mazingira yanayozunguka. Suala ni kuitangaza Zanzibar duniani kote, kuimarisha maeneo ya kihistoria pamoja na kukiimarisha Chuo cha Maendeleo ya Utalii vitapewa kipaumbele.

Mhe. Spika, Sekta ya Viwanda nayo itapewa msukumo maalum na kuendelezwa hasa viwanda vidogo vidogo na viwanda vya kati. Kwa hivi sasa sehemu kubwa ya viwanda hivi vipo katika sekta isiyorasmi vikijihusisha na kazi ndogo ndogo. Kama vile useremala, ufuaji wa bidhaa za chuma, ufundi wa gereji, ufinyanzi na ufumaji. Ufanisi na tija kazi hizo bado ni za chini sana.

Lengo la serikali ya awamu ya saba ni kufanya sensa katika sekta hii, kuwa na taarifa ya muundo mkubwa sana, aina ya teknolojia, bidhaa zinazozalishwa na ajira inayopatikana. Taarifa hizo zitaiwezesha serikali yangu kuandaa mpango wa kuwasaidia wajasiliamali wa sekta hiyo, kwanza kwa kuwa na vifaa bora vya kufanyia kazi, mafunzo juu ya ubora wa bidhaa, upatikanaji wa mitaji, upatikanaji wa masoko na uongozi wa viwanda kwa jumla.

Kustawi kwa sekta ya viwanda vidogo na vya kati kutapatiwa fursa za ajira kwa vijana kuingiza teknolojia mpya na kujenga uhusiano wa kutegemeana na sekta nyengine, hasa sekta ya biashara. Mkazo mkubwa utawekwa katika viwanda vinavyotumia malighafi inayopatikana hapa Zanzibar na Tanzania Bara. Kama ilivyoelezwa katika ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mapinduzi ya Viwanda na Biashara yatakwenda sambamba na uimarishaji wa maeneo yote ya EPZ ya Fumba na Micheweni, viwanda vidogo vidogo vya Amani kwa kuijengea miundombinu na kuwashajihisha wawekezaji wa nje na wa ndani wawekeze katika maeneo hayo.

Tutawashajihisha ndugu zetu wa Tanzania wanaoishi nchi za nje, wanaoishi uhaibuni kwa jina maarufu la Dayafra, ili nao waje wawekeze nchini kwao. Wameanza kushughulikia suala hili kupitia Wizara ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ambapo tumeanzisha kitengo Dayafra, tatawashajihisha ndugu zetu hawa wenye uwezo, wao wenyewe , waje wawekeze au kwa kushirikiana na wawekezaji wengine wa ndani ya nchi na wale walio nje ya nchi kwa kutegemea taratibu, sheria na mipango ya nchi yetu.

Mhe. Spika, sekta ya kilimo ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi na maendeleo ya Zanzibar. Kilimo ndicho chanzo kikuu cha ajira kwa wananchi waliowengi zaidi hasa vijijini na inachangia asilimia 27.3 ya pato la taifa katika uchumi wetu, na kutoa ajira kwa wastani wa asilimia 44 ya wananchi wa vijijini. Kwa kutambua umuhimu wa mchango wa sekta ya kilimo katika kujenga msingi wa uchumi wa kisasa.

Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali ya Umoja ya Kitaifa ya Awamu ya Saba nitakayoiongoza nitatekeleza mambo yafuatayo;

Nitasimamia utekelezaji wa sera na programu mbali mbali za kilimo na kuzifanyia mapitio kwa lengo la kuzifanyia mapitio kwa lengo la kuziimarisha. Aidha, serikali itaandaa sera ya chakula na liche na sera ya mifugo, nayo kadhalika zitaimarishwa.

Nitaendelea kuhimiza na kutia mkazo mafunzo ya matumizi ya kanuni za kilimo bora, kwa mazao ya chakula, mazao ya biashara na matunda. Huduma za ugani na zana za kisasa za kilimo, wanyama wa kazi, matrekta makubwa na matrekta madogo. Mwaka jana tuliagiza nchini matrekta makubwa 27 na matrekta madogo 20. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, tutahakikisha tunaongeza maradufu zaidi matrekta hayo.

Tutaongeza miundombinu ya umwagiliaji maji na kuhakikisha kwamba uvunaji wa maji ya mvua, ili yatumike katika kuyazidisha mazao mengi zaidi ya chakula na mboga kutokana na umwagiliaji maji.

Tutahakikisha kwamba sekta binafsi inatoa huduma za pembejeo katika maeneo ya kilimo.

Tutaendelea kukiimarisha Chuo chetu cha Kilimo kilichopo Kizimbani na kuendeleza utafiti wa mbegu bora za mazao ya chakula na biashara. Njia ya utafiti shirikishi itatumika kwa lengo la kuwawezesha wakulima ili waweze kushiriki kikamilifu katika kutoa mawazo yao kuhusiana na matatizo yanayowakabili.

Tutaanzisha mradi maalum wa kuwawezesha wananchi na sekta binafsi, iingie katika kilimo cha kisasa na kilimo cha biashara ya mazao ya viungo na matunda ya nchini kwetu.

Tutajitahidi sana kuendeleza vituo vya huduma na udhibiti wa maradhi ya mazao na wadudu waharibifu. Tutaiendeleza kwa kasi sana elimu kwa wakulima. Kuhusu hifadhi ya mazao ni utafutaji wa masomo ya ndani na nje ya

nchi, ili kuitumia nembo ya Zanzibar ifanye kazi zaidi. Maeneo yote hayo yanayohusu kilimo yatashughulikiwa ipasavyo katika serikali yangu ya awamu ya saba.

Katika suala la ajira hapa nchini ni suala muhimu sana, kama nilivyokwisha kueleza kwamba hivi sasa zaidi ya asilimia 40 ya watu wote wenye uwezo wa kufanya kazi wameajiriwa na sekta ya kilimo. Hata hivyo, ajira yenyewe bado haitoi tija zaidi na inatarajiwa kufanyika kazi kubwa yenye kuwavutia vijana ambao ndio waliowengi na wenye uwezo wa kufanya kazi.

Lengo la dira ya Zanzibar ya 2020, ni kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2020 asilimia 50 ya watu wenye uwezo wa kufanyakazi wawe wameajiriwa kama nilivyosema awali, katika sekta ya utalii. Vile vile asilimia 20 wawe wameajiriwa na sekta ya kilimo na asilimia 30 wawe wameajiriwa kwenye sekta nyengine mbali mbali. Matarajio haya yatafikiwa tu iwapo tutaweza kuyatekeleza barabara malengo ya mageuzi ya uchumi katika sekta za utalii na viwanda kama nilivyoeleza hapo awali.

Ni muhimu hata hivyo tukahakikisha kwamba sekta binafsi inapata msaada na kuwezeshwa kupanuka na kuwa ndio chanzo kikuu cha ajira hapa nchini. Serikali kwa upande wake itachukua juhudi ya kushirikiana na Jumuiya ya Wafanyabiashara wenye viwanda na wakulima, ili kubudi programu zitakazoimarisha sekta binafsi.

Aidha, kwa kupitia Baraza la Biashara la Zanzibar ZBC, serikali ya awamu ya saba itahakikisha kwamba inatoa ufumbuzi wa haraka kwa changamoto zilizokwishakutoa maendeleo ya sekta binafsi hapa nchini. Ajira ni matokeo ya soko, mbinu sahihi za kukuza ajira ni kujenga mahitaji na kuandaa nguvu kazi kulingana na mahitaji yaliopo.

Katika kupambana na umaskini, juhudi katika eneo hili pamoja na mambo mengine Serikali ya Mapinduzi ya Awamu ya Saba itatekeleza mambo yafuatayo.

Tutaendeleza mafunzo ya ujasiriamali kwa wananchi na kuhamasisha matumizi ya kanuni za kilimo bora na sayansi na teknolojia, ili iwe rahisi zaidi katika uzalishaji mali.

Tutaendeleza utekelezaji wa awamu ya tatu ya mkuza.

Tutaimarisha mifuko ya uzalishaji na kuwawezesha wananchi kiuchumi, ili kukuza uwezo wao na kutoa mikopo kwa wananchi na kuwawezesha kutumia fursa zilizopo katika maeneo wanayoishi ili kujiendeleza kiuchumi.

Uanzishwaji wa vikundi vya SACOS haza kwa vijana na kinamama, uendelezaji wa maeneo maalum ya kufanya shughuli zao za biashara ndogo ndogo, pamoja na kutambua rasilimali za biashara za wanyonge ambazo ziko katika sekta isiyorasmi, zitafanyiwa kazi kikamilifu katika serikali yangu ya awamu ya saba.

Kuhusu miundombinu, ustawi wa uchumi unakwenda sambamba na maendeleo ya uchumi kama vile barabara, bandari, viwanja vya ndege, maeneo huru ya uzalishaji na mazingira. Kama nilivyoeleza hapo awali juhudi kubwa iliyochukuliwa na uongozi wa awamu ya sita katika kujenga na kuimarisha miundombinu ya kiuchumi na kijamii hapa nchini, basi jitihada hizi zitaendelezwa katika serikali yangu ya awamu ya saba.

Jitihada zilizofanywa na awamu ya sita zimewezesha asilimia 70 ya barabara zote za Unguja na Pemba zimejengwa kwa kiwango cha lami na barabara nyingi za mjini nazo zinafanyiwa matengenezo makubwa na mji wetu kupengeza.

Kuhusiana na barabara, serikali yangu itakuwa na majukumu matatu makuu. Jukumu la kwanza, ni kuhakikisha kwamba barabara zote kuu zilizobaki zenye kiwango cha asilimia 30 zinakamilishwa katika kipindi kifupi kijacho.

Jukumu la pili, ni kuhakikisha kwamba tunazijenga kwa kiwango cha kupitika kwa mwaka mzima hasa zile barabara ndogo ndogo za ndani ya maeneo yetu tunayoishi, mjini na mashamba. Kazi hii itafanyika kwa wakati mmoja kwa Unguja na Pemba.

Kukamilika kwa hatua hii kutasaidia kuyafungua maeneo ya ndani ya nchi yetu ili yaweze kutumika vizuri kiuchumi na njia hizo ndizo zitakazoinua thamani ya barabara zetu.

Jukumu la tatu, ni kuhusu sekta hii, ni suala zima la utunzaji wa barabara na matengenezo yake kila zinapoharibika. Hili ni suala muhimu sana na jukumu hili hatuna budi tulitekeleze vizuri kwa kuviimarisha vikosi vyetu viliopo kwa matengenezo ya barabara zetu, mjini na vijijini.

Katika usafiri wa anga. Mhe. Spika, tunatambua kuwa usafiri wa anga ni moja ya nyenzo muhimu katika kukuza uchumi. Kazi ya matengenezo makubwa ya njia ya kurukia ndege kwenye uwanja wa ndege wa kimataifa wa Karume Zanzibar zimekamilika. Uwanja huu hivi sasa una uwezo wa kutumikia ndege kubwa mchana na usiku. Kazi iliyotukabili katika kiwanja hicho, ni kuanza kukamilisha ujenzi wa majengo ya maeneo ya usafiri wanaoingia na kuondoka

ikiwa na huduma zilizobora zaidi na za kisasa. Mkandarasi kwa ajili ya kazi hii tayari amepatikana na kazi itaanza muda si mrefu ujao.

Kuhusu Kiwanja cha Karume cha Pemba, lengo pia ni kukifanya kiwanja hicho kiweze kutumika usiku na mchana. Kujenga mtandao wa taa za uwanjani wenye kuaminika, ili ndege ziweze kutua wakati wowote. Mpango wa kazi tayari upo na kazi itaanza mara tu utaratibu utakapomalizika katika serikali ya awamu ya saba.

Aidha, tutaupanua Uwanja wa Karume wa Pemba. Vile vile tutaongeza ufanisi wa kazi kwa wafanyakazi, watapatiwa mafunzo na huduma za zimamoto zitaimarishwa kwa Unguja na Pemba.

Kuhusu bandari, nchi yetu inategemea sana usafiri wa baharini kwa shughuli zake mbali mbali. Kwa hivyo, bandari za kisasa ni jambo lisiloweza kuepukika. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwamba kazi kubwa ya kukarabati ujenzi wa bandari kuu ya Malindi imekamilika na bandari hiyo sasa inatumika kwa ufanisi.

Licha ya kukamilika kwa bandari kuu ya Malindi. Kukua kwa mji wa Zanzibar una msongamano unaojitokeza bandarini, kwa shughuli za upakiaji na uteremshaji wa mizigo pamoja na abiria umepelekea haja ya ujenzi wa bandari mpya ya mizigo. Lengo pia ni kutumia bandari hiyo kwa kuidhihirishia Zanzibar katika ramani ya biashara kikamilifu, kwa kushajihisha biashara ya mpito, yaani *transit trade*.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba itaendeleza mchakato wa maandalizi ya ujenzi wa bandari mpya ya mizigo katika eneo la Mpigaduri Maruhubi. *(Makofi).*

Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Awamu ya Saba itajenga majengo mapya ya Bandari ya Malindi pamoja na maeneo ya kuhifadhi makontena na kuviimarisha vifaa katika bandari hiyo. Pia kuimarisha gati ya Mkokotoni na kuwajengea jeti kwa ajili ya vyombo mbali mbali vya baharini, pamoja na ujenzi wa jeti ndogo kule Tumbatu. Ujenzi wa jeti ndogo halikadhalika tutaijenga kule Chokocho kwa wasafiri kwenda Kisiwapanza *(Makofi).*

Kwa upande wa Pemba vile vile bandari ya Mkoani itafanyiwa matengenezo makubwa kwa kurekebisha sehemu ya gati iliyodidimia na kuipatia vifaa vya kuhudumia mizigo vya kisasa. Kadhalika gati ya Wete pia itaongezwa urefu na upana wake na kuipatia vifaa vya kuhudumia mizigo na wananchi.

Kuhusu umeme, nishati ya umeme kama nilivyosema imefikia kiwango kizuri katika nchi yetu. Katika kipindi kijacho tutahakikisha maeneo yote ya mjini na vijijini ambayo bado hawajapata nishati ya umeme yanaendelezwa na kuhakikisha kwamba umeme unafika katika maeneo.

Serikali ya Awamu ya Saba itapeleka umeme katika visiwa, tutahakikisha kwamba tunapeleka umeme katika Kisiwa cha Makoongwe Mkoani, Kisiwa Panza na Kisiwa cha Shamiani.

Mhe. Spika, huduma za jamii. Miundombinu za huduma ya jamii ni pamoja na ile ya elimu, afya na huduma za maji safi na salama. Nimeyataja maeneo haya kwani yanahitaji hatua maalum. Elimu inajumuisha kukuza rasilimali watu ya nchi yetu, kama nilivyosema awali na msingi wake unaanzia katika kutoa elimu tangu utotoni na kuendelea hadi vyuo vikuu.

Serikali ya Awamu ya Saba, katika mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, inakusudia kukuza na kuendeleza maendeleo yaliyopatikana katika nchi yetu katika sekta ya elimu. Ili kuendeleza elimu, mipango itahusisha maendeleo ya elimu zote, tangu elimu ya maandalizi, msingi, sekondari, vyuo pamoja na elimu ya amali na elimu mbadala.

Nia ya Serikali ya Awamu ya Saba ni kuongeza ubora wa elimu katika elimu za msingi na sekondari, na kuhakikisha kwamba watoto wote waliofika umri unaostahiki basi wanapata elimu hiyo. Katika kufanikisha haya tutahakikisha kwamba watoto wote wenye umri wa miaka 6 hadi 11 wanapatiwa elimu ya msingi iliyobora. Tutaimarisha mafunzo ya walimu na kuhakikisha kwamba walimu wanapatiwa elimu bora zaidi na wanahamasishwa kubaki kazini kwa kupatiwa maslahi bora. (*Makofi).*

Nafasi za elimu pia zitaendelea kutolewa kwa watoto wenye ulemavu hasa kwa kujumuishwa na wenzao katika elimu ya kawaida, serikali yangu inatambua na kuthamini sana kwamba elimu ni haki ya kila mtoto bila ya ubaguzi wa aina yoyote ile, pia tunatambua kwamba jamii iliyoelimika ni raslimali ya taifa na ndio nguvu kazi na usukani wa maendeleo yetu. Napenda nirudie elimu bora itakuwa ndio lengo letu kuu katika elimu zote ikijumuishwa teknolojia ya habari ya mawasiliano, kwa kuzipatia skuli zetu kompyuta ili watoto wetu waweze kujifunza na teknolojia ya mawasiliano ya habari ya leo, tutawapatia vitabu kwa kila mwanafunzi wa Kidatu cha Kwanza hadi cha Sita awe na kitabu kwa somo linalohusika. Tutaimarisha masomo ya sayansi na hesabu na kuweka mazingira bora ya skuli hasa za msingi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tutawashajihisha sana ndugu zetu watoto wa kike ili nao wasome masomo ya sayansi na teknolojia, mipango itaendelezwa ya kujenga skuli mpya

za sekondari na nyumba za walimu Unguja na Pemba, tuna mpango mkubwa wa skuli ishirini na moja kupitia Benki ya Dunia ziatajengwa Unguja na Pemba na skuli za sekondari nilizoziieleza katika kampeni yetu kwa kila eneo na program zitaandaliwa kwa kufafanua na kusimamia suala hili.

Lakini vile vile tutajenga nyumba za walimu na kwenda sambamba na skuli mpya zitakazojengwa, serikali yangu katika miaka ijayo itahakikisha kwamba inasimamia na kukamilisha mradi mkubwa wa kuokoa maisha ya elimu ya lazima unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Kadhalika ndugu zetu wa benki ya nchi za Kiarabu *(BADEA)* nao wametuunga mkono kwa kujenga skuli mbili za mfano kubwa Unguja na Pemba.

Katika kukamilika kwa mradi huu wa Benki ya Dunia kutaongezwa ubora wa skuli zetu majengo na vifaa, skuli zote za sekondari tutahakikisha tunazijengea maabara kwa ajili ya kazi za majaribio Mkoa kwa Mkoa. *(Makofi).*

Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi napenda kuwapa habari zilizo rasmi ambazo wenzetu wanazita *break news* kwamba hivi ninavyosema katika bandari yetu Zanzibar tayari tumepokea makontena yanayokadiriwa kwamba yana zana za maabara za skuli zisizopungua thalathini na saba za sekondari kwa kuazia. Huu ni mwanzo tu wa safari yetu ndefu ya kuziimarisha maabara za skuli zetu za sekondari tumuombe Mwenyezi Mungu azidi kutusaidia ili tufanikiwe.

Mhe. Mwenyekiti, Ujenzi wa Chuo Kiku cha Taifa yaani SUZA nao tumeanza kuushughulikia na katika awamu zote awamu uliyopita na awamu ijayo ninahakikisha kazi kubwa itafanywa katika ujenzi wa chuo huki. Nia ya serikali yetu kuimarisha ubora wa elimu na kuona kwamba watoto wote hapa nchini wanafaidika na elimu ya juu bila ya ubaguzi wa aina yoyote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu mambo ya kale nchi yetu ina historia na rekodi kubwa ya mambo ya kale ni muhimu kuyahifadhi, kuyaendeleza na kutunza kumbukumbu na mambo yote ya kazi ili kuwepo kwake kunufaishe watu wetu, watalii na wanahistoria, na wale mabingwa wa kiolojia mbali mbali duniani ili waje wajifunze kwetu na kuendeleza nchi yetu ya Zanzibar iendelee kusifika na kutajika katika medani za kumbukumbu za dunia. Katika kufanya hivyo tutaimarisha makumbusha na kuandaa mipango ya miaka mitano ya hifadhi ya mambo ya kale pamoja na kuendeleza ukusanyaji wa kumbukumbu na nyaraka katika afisi ya serikali na kuzihifadhi ipasavyo.

Mhe. Spika, katika afya tumeshasisitiza sana utoaji wa huduma bora za afya kama tulivyosisitiza huduma bora za elimu tunasisitiza sana kwa elimu bora za afya kwa wananchi wote bila ya ubaguzi wowote, kwani afya bora ni moja ya

malengo ya mapinduzi matukufu ya Januari, 12 mwaka 1964. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba katika mfumo mmoja wa kitaifa imekusudia kuimarisha huduma za afya kwa kuhakikisha kwamba tunatekeleza kwa vitendo katika kipindi hiki sera ya afya na kushirikisha wananchi katika utekelezaji wa sera hiyo, katika mnasaba huu hospitali yetu ya Mnazi Mmoja tutahakikisha tunakamilisha utaratibu tuliouandaa kipindi kirefu kilichopita cha kufanya hospitali hii kuwa ya rufaa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tutaziimarisha huduma za kinga na huduma za afya za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii huku tukizingatia vitengo maalum kuvianzisha na vyengine kuvipa nguvu, tuna lengo la kuanzisha utibabu wa huduma za maradhi ya kensa, tuna lengo la kuimarisha upasuaji wa ubongo ambao tumesaidiwa na ndugu zetu wa Hispania, tutawafundisha wataalam wetu na mabingwa wetu tufanye vizuri zaidi kwa maeneo haya. Tuna lengo ya kuanzisha vitengo vya kushughulikia maradhi yanayotokana na matatizo ya figo na maradhi ya moyo kwamba zile kesi ambazo tunazipeleka nje kwa matibabu nia yetu tuweze kuzihudumia wenyewe hapa hapa nyumbani, tumeanza kuchukua hatua kwa kupata vifaaa vya kisasa vya uchunguzi wa maradhi ambao ndio jambo kubwa kwa matibabu ya mwanadamu, kwa sababu unapochunguza maradhi na kuyabaini utibabu wake haukusumbui sana, tutajiimarisha sana katika jitihada zetu za kuhudumia huduma za uchunguzi wa maradhi.

Kadhalika Mhe. Spika, hospitali yetu ya Abdalla Mzee ile ya Mkoani na Hospitali ya Wete tutazipandisha daraja kuwa hospitali za mikoa na ile hospitali yetu ya Vitongoji ya *Cottage* ya Kaskazini (A) pale Kivunge na ya Makunduchi tutazipandisha daraja ziwe hospitali za Wilaya, kwa kufanya hivyo huduma za afya tutaziimarisha sambamba na kuimarisha vituo vya afya kuzipa nyenzo vifaa, dawa za kutosha kila pahali ambapo uwezo wa serikali unapoimarika hatutopenda wananchi wetu walalamikie huduma zetu za afya tutajitahidi sana kuwaelekeza watumishi wa Wizara ya Afya na Ustawa wa Jamii wazingatie maadili ya fani zao kwa madaktari na wauguzi maadili haya yanawaelekeza watumikie wananchi bila ya woga, bila ya hofu na bila ya upendeleo, waswahili wanasema lugha nzuri humtoa nyoka pangoni. *(Makofi)*

Lakini na mimi naamini kwamba ndugu zangu na wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii wana uwezo mkubwa kwa kutumia maadili ya fani zao ili kuwaridhisha wagonjwa wetu watakaofika hospitali zetu. Serikali ya Mapinduzi ya awami ya saba kadhalika itaendelea kumarisha huduma za kinga katika hospitali zote na katika vituo vyote vya afya na kusisitiza zaidi elimu ya afya kwa wananchi ili kuyadhibiti maradhi hasa ya kuambukiza. Mapambano dhidi ya maradhi ya malaria, UKIMWI na maradhi mengine fakiri ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukizwa yataendelezwa na kushughulikiwa

katika uwezo wote wa serikali yetu lakini jambo la msingi ni huduma za tiba asili nazo zitapewa msukumo mkubwa katika sehemu zote za nchi yetu kwa Unguja na Pemba huku tukiimarisha Chuo chetu cha Taaluma za Sayansi za Afya pamoja na kuwapatia mafunzo wataalam wa afya ndani ya nchi na nje ya nchi na kuimarisha maslahi yao kwa kadri ya uwezo wa serikali.

Katika huduma za jamii tunahusika vile vile katika serikali yetu kuziimarisha huduma za upatikanaji wa maji safi na maji salama na ili kuendeleza kazi hiyo ya usambazaji wa maji safi na maji salama kwa wananchi, serikali yetu ya awamu ya saba tutahakikisha kwamba tunakamilisha awamu ya pili ya mradi wa usambazaji maji na salama katika Mkoa wa Mjini/ Magharibi. Tumefikia katika hatua nzuri sana ndugu zetu wa Serikali ya Japan wametusaidia sana mambo ya msingi wameyakamilisha yaliyobaki ni mambo ambayo tunapaswa sisi tuyatekeleze katika kipindi kifupi kijacho, suala hili tutalikamilisha na tatizo la maji Mkoa wa Mjini/Magharibi litakuwa ni historia.

Mhe. Spika, tutahakikisha kwamba upotevu wa kiwango cha maji kwa kufunga mita za maji na kuelimisha wateja wetu wanaopata huduma za maji kutumia vizuri ili waweze kuhifadhi, tutaandaa sera zilizo safi sana kwa ajili ya usafi wa mazingira ili kuweza kudhibiti kwa kiwango kikubwa sana ikiwemo kusimamia vyema shughuli za maji machafu na hili linakwenda sambamba na usafi wa wingi wa umoja, tutaendelea kusambaza maji safi na salama kutoka asilimia sabini na tano hivi kutoka katika miji hadi kufikia asilimia tisini na tano katika mwaka 2015, vijijini kutoka asilimia sitini hivi sasa na kufika asilimia thamanini hadi mwaka 2015.

Mhe. Mwenyekiti, tunatarajia kupokea mradi mkubwa kabisa wa maji kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa Mji wa Wete, Chake-Chake na Mkoani utafaidika sana na mpango huu na miji mengine na vijijini vyengine kama katika Wilaya ya kati kwa Unguja.

Kuhusu makaazi serikali yetu itaendeleza upatikanaji wa makaazi bora kwa watu wote tutashirikisha na kushirikiana na sekta za watu binafsi na wananchi katika kufanikisha lengo hili la kujenga nyumba bora zaidi. Wakati huo huo nataka nirudie tena suala la usafi wa mazingira kwa Manispaa ya Unguja, sote hatufurahishwi na usafi wa mji wetu mamlaka ya Mji Mkongwe, Baraza La Manispaa la Zanzibar lazima visimamie kwa umakini mkubwa sana usafi wa mazingira. Taratibu na sheria zilizoagizwa kutekeleza hilo watapaswa walishughuliki. Mji wa Zanzibar usiku haupendezi una giza sana tutazifufua taa zote za barabarani tunataka wananchi wetu watembee usiku na mchana kwa furaha na waringe katika mji wao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika michezo nasema inakuza ustawi wa jamii na michezo ni afya. Nia ya serikali yetu ya awamu ya saba ni kukuza na kuendeleza michezo nchini, kutoa mafunzo kwa wanamichezo na njia nyengine ni kuikuza sekta hii kama vile kusaidia timu zetu za mpira wa miguu, mbio na nyenginezo na kushiriki kikamilifu katika mashindano ya kimataifa. Katika kipindi kijacho ni matarajio ya serikali yetu kwamba Zanzibar itakuwa ni mjumbe wa *FIFA*. Jitihada zilizofikiwa na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa hivi sasa ni kubwa ujumbe wetu uliokwenda Geneva mwaka huu umefanya kazi kubwa kwa kuzungumza na Bwana Sept Blatter matumaini ni makubwa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu tuvuke katika jambo hili. *(Makofi)*

Nasena tutaendeleza michezo yote inayochezwa sasa hivi na ile ambayo imesahaulika kuchezwa au inachezwa kwa kiwango cha chini kama vile *Golf*, *Cricket*, *Table Tennis* na mengineyo, lakini vile vile serikali yangu itahakikisha kwamba suala la utamaduni mila na silka zetu zinapewa kipaumbele kama vile burudani, taarab asilia tutaziendeleza ili watu wengi waje kujifunza taarab asilia Zanzibar na wasanii wetu maarufu, vijana kwa wazee tutawatunza na kuwaenzi ili iendelee kuwa hazina ya nchi yetu, tutafanya kila jitihada tuwajengee studio ya kisasa ya kurikodia mambo yao. *(Makofi)*

Kuhusu vyombo vya habari tunaelewa umuhimu wa habari na tunaelewa umuhimu wa vyombo hivyo, tutaendeleza kuwapa uhuru wa kuendeleza vyombo vya habari, katika kipindi hiki tutasimamia sana sera ya habari kanuni na miongozo na sheria ya habari ili tuweze kuongoza kwa ufanisi zaidi na kuleta mageuzi ya utangazaji nchini, vyombo vyetu vya habari vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Televisheni na Radio na Magazeti tutavipa nyenzo na vyombo vya kisasa ili viweze kufanya kazi zake vizuri na visikike nje ya nchi yetu.

Mhe. Spika, katika kuendeleza makundi mbali mbali jamii na mkusanyiko wa watu mbali mbali kwa mfano vijana, wazee na watoto, wanawake na wanaume makundi haya hayana budi na huwa yanahitaji kuendelezwa ambapo nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuendeleza ipasavyo. Katika awamu ya saba ya serikali ya umoja wa kitaifa inatambua kwamba wanawake ni watu wenye uwezo mkubwa na wana nguvu kubwa katika kupeleka mbele kasi ya maendeleo ya kiuchumi kijamii na kisiasa. Tunaamini kwamba wanawake wakiwezeshwa wanaweza hilo ndilo litakuwa lengo la serikali ninayoiongoza, mipango na sera madhubuti ya kuwapatia wanawake msukumo wa kifedha kupitia mifuko mbali mbali itawekwa, katika kuimarisha mifuko hii iliyopo tutafanya jitihada kuanzisha benki ya wanawake Zanzibar ni jambo la faraja kuona uwakilishi wa wanawake katika Baraza la Nane umeimarika sana kwa kuwa na wajumbe wanawake ishirini na mbili.

Hii ni nguvu kubwa sana na inaelekea kuwepo lengo na uwiano wa asilimia hamsini, maratajio yangu kuwa wajumbe hawa watakuwa mbele sana katika kuchochea maendeleo ya wanawake na jamii kwa jumla, nitawaendeleza watoto kwani watoto ndio chanzo cha raslimali watu na umiliki wa taifa letu tunaamini kwamba watoto wana haki ya kuishi, wana haki ya kulindwa na kuendelezwa na kupewa elimu ya afya na hasa afya bora na kutobaguliwa kwa mujibu wa katiba na sheria ya nchi yetu, hii ndio imani kubwa ya serikali ninayoongoza kuhusu watoto na jukumu letu ni kuhakikisha kwamba utekelezaji wa mipango ya kuwanufaisha na kuendeleza watoto wetu katika nchi yetu hivyo hivyo kwa walemavu.

Mhe. Mwenyekiti, tunaamini sana na tunathamini usawa wa binadamu na katika hilo natambua kwamba walemavu wanayo haki sawa na binaadam wengine wote kama vile walivyokuwa nayo binaadam wengine kwa mujibu wa katiba yetu, lakini pamoja na hayo wanayo haki ya kuendelezwa kuheshimiwa na kutokubaguliwa na tunatambua kwamba wenye ulemavu wana uwezo wa kushiriki katika uchumi wa jamii. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuwapatia fursa za mafunzo stadi mbali mbali, elimu na uwezo wa kupata misaada wa mikopo ya kifedha na vifaa vya kisasa kwa kuwasaidia na kujiendeleza, kadhalika serikali itaendelea kushirikiana na kuiunga mkono Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu na kuimarisha ustawi wake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, suala la vijana nalo litashughulikiwa na serikali yangu ya awamu ya saba katika mnasaba ule ule kama watavyoshughulikiwa akinamama, watoto na walemavu kwani vijana ndio nguzo pekee ya siasa na uchumi wa jamii, tunaelewa kwamba vijana walioandaliwa vyema na kujipanga vizuri wana mchango mkubwa sana katika kukuza uchumi na maendeleo ya jamii. Tunatambua kwamba changamoto zinazowakabili vijana zikiwemo ukosefu wa ajira na mitaji ya kujiendeleza, katika kusaidia vijana kupambana na changamoto hiyo serikali itaanzisha mfuko maalum wa vijana utakaotoa mikopo nafuu ili wajiendeleze katika shughuli za kiuchumi na kujipatia ajira pamoja na kuzidisha usishirikiano wao na hasa sehemu zilizokuwa sio za serikali zenye kushughulikia maendeleo ya vijana, tutasimamia utekelezaji wa sera ya maendeleo ya vijana na kushughulikia zaidi juu ya suala la ajira zao pamoja na hayo katika kipindi hiki serikali yangu itahakikisha inaanzisha Baraza la Vijana la taifa ambalo litaimarisha ushiriki wao katika ngazi mbali mbali za maamuzi, kwa kupiga vita ukimwi na mapambano dhidi ya madawa ya kulevya.

Wazee ni hazina na chem chem ya busara katika jamii yetu tutawastawisha na kuwaendeleza wazee wetu na kuendeleza utamaduni wa kuwaenzi na kuwatunza na kuwapenda wazee wetu, tutawapa misaada mbali mbali ya mahitaji ikiwemo huduma za afya na nyenginezo.

Mhe. Spika, kuhusu wafanyakazi ni raslimali kubwa moja katika nchi yetu ni wafanyakazi ambao ndio msingi wa kujenga uchumi na maendeleo ya nchi yoyote ile duniani, kwa upande wa utumishi serikalini tayari serikali imeidhinisha utekelezaji wa program maalum ya *management* ya utumishi wa umma, program hii inafafanua majukumu ya watendaji serikalini, suala la mgawanyo wa mamlaka na dhamana na nidhamu ya uwajibikaji wa kazi, viwango vya malipo na haki nyengine za utumishi. Wafanyakazi watawajibika kuishi na kuwajibika kufanya kazi kwa mujibu wa kanuni za utumishi, serikali kwa upande wake itachukua dhima ya kuelimisha watumishi wake wote juu ya kanuni hizo za utumishi haki na wajibu wao. Serikali pia itahakikisha kwamba inaandaa mipango mahususi ya maendeleo ya watumishi.

Kila Wizara itawajibika kuwa na mpango wake wa mafunzo kwa wafanyakazi na mafunzo mpango unaofahamika ambao utapaswa utekelezwe kwa ajili ya mafunzo ya muda mrefu na mafunzo ya muda mfupi na mafunzo ya muda wa kati ili kuwapa nyenzo na uwezo wafanyakazi kuyafahamu maeneo yao ya kazi na kutumika ipasavyo, maslahi bora ya wafanyakazi popote pale ni ajenda yetu na tunaimarisha mashirikiano na chombo chao na vyombo huru vya wafanyakazi ili kukuza mahusiano yaliyopo katika kuendeleza wafanyakazi. Serikali yangu itaimarisha mazingira bora ya kazi na maslahi ya wafanyakazi kwa kadri hali ya uchumi wetu na kadri uchumi unavyoimarika.

Suala la miundo ya watumishi yaani *scheme of service* itashughulikiwa kwa kadri ya kada za utumishi zilivyo, kuna nia katika serikali yangu ya kuanzisha Wizara ya Utumishi wa Umma ambayo pamoja na mambo mengine itahusika na mambo yafuatayo.

1. Maadili kwa wafanyakazi pamoja na kuzielewa sheria za utumishi na kuelimishwa vizuri.
2. Kila Wizara itakuwa na mpango wake wa mafunzo wa uhakika kama nilivyoeleza ili wafanyakazi wajue wanachokifanya wakiwa kazini hatutaki wabahatishe, wala hatutaki kuwalaumu tunataka kuwapa nyenzo na pale watakaposhindwa ndipo tutakapowalaumu tena.

Suala la maslahi ya wafanyakazi nataka niahidi nitalishughulikia katika kipindi kifupi kinachokuja ili tuone namna ya kuimarisha maslahi ya mfanyakazi hatua kwa hatua na kwa kila kada.

Mhe. Spika, mambo yote niliyoyasema yanahitaji utulivu na amani ya nchi yetu, amani na usalama kwa watu wote, lakini pia usalama kwa mali zao.

Serikali ya Mapinduzi ya Awamu ya Saba kwa mujibu wa katiba yake imeanzisha idara maalum, zamani ikiitwa vikosi maalum kwa shughuli hizi za usalama. Vikosi hivi vinastahiki pongezi kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutunza amani na usalama wakati wa mchakato wote wa uchaguzi wakishirikiana na vikosi vyetu vya taifa vya ulinzi, polisi na jeshi la wananchi wa Tanzania katika shukrani, nasema ahsanteni sana vikosi vyetu kwa kazi nzuri.

Katika Awamu hii ya Saba, serikali yetu itaendelea kuviimarisha vikosi maalum kwa kuvipa taaluma, kuvipa vifaa bora vya kisasa na kazi zote zikiwemo za ulinzi na kukuza uchumi. Idara Maalum za Serikali ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu. Serikali itasaidia sana katika utekelezaji wa mipango ya kila idara katika Idara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Lakini suala la kudumisha amani sio la idara maalum peke yake, lakini wale wanashirikisha zaidi wananchi wote kwa jumla.

Leo tunajivunia utulivu ndani ya nchi yetu. Msingi wake ni kudumishwa kwa amani na mimi natamka wazi wazi kama nilivyosema mara zote, sitomvumilia yeyote atakayethubutu kwa kujaribu kuvunja amani ya nchi yetu. Nchi yetu imepata sifa kubwa sana ya amani, hasa kutokana na maridhiano yaliopo, baada ya kukutana kwa viongozi wetu wawili Mhe. Dk. Aman Abeid Karume na Maalim Seif Sharif Hamad *(Makofi).*

Hata Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendeshwa kwa sera zinazopendelea amani na utulivu. Tunawajibu wa kuyalinda maridhiano hayo ambayo ndio chachu ya amani yetu na kuikuza iwe ni nguvu kubwa ya kudumisha Mapinduzi yetu ya Zanzibar ya mwaka 1964. Vile vile amani hiyo iwe ni chachu kubwa sana ya kuimarisha Muungano wetu wa Tanzania.

Kama tunavyofahamu marekebisho ya 10 ya Katiba ya Zanzibar yameipatia hadhi kubwa sana nchi yetu mbele ya wananchi wa Zanzibar na Tanzania na mbele ya Jumuiya ya Kimataifa. Aidha marekebisho hayo, yamedhihirisha kuwa tunaweza kuweka mbele maslahi ya nchi yetu hii dhidi ya maslahi binafsi, na kwamba sisi tulio Wazanzibari tunaweza kutatua matatizo yetu wenyewe bila ya kupata msukumo wowote kutoka nje ya nchi, ili tumelidhihirisha kwa vitendo.

Marekebisho haya ya Katiba ya 10 yamekuwa ni kielelezo cha uungwana, na yameweka mwamko mpya wa kushirikiana baina ya vyama vyetu vikuu vya siasa pamoja na wananchi wetu kwa jumla. Jamii yetu sasa imepata mwangaza mpya wa matumaini. Jamii yetu imepata masikilizano na hivyo kutoa fursa thabiti ya kujenga na kuimarisha nchi yetu kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Mhe. Spika, suala la maadilini ni suala la utawala bora, na suala hili ndio itakuwa ajenda yetu ya kitaifa. Suala hili linamuhusu kila mmoja wetu aliyekuwa kiongozi, kwa wale waliochaguliwa, watakaoteuliwa na watakaoteuliwa baadae. Tunapaswa basi kwa hivyo tuwajibike kwa wananchi waliotuchagua ili maadili yanayohusu wananchi nayo yazidi kuimarishwa.

Katika suala hili la demokrasia na utawala bora na maadili, rushwa ni suala mojawapo linalohusu maadili ya viongozi. Watumishi serikalini lakini pia na wananchi kwa jumla. Nataka niwahakikishie wananchi wote wa Zanzibar kwamba tutapambana na rushwa kwa hali yoyote ile. Hatua moja kubwa tutakayochukua ni kushughulikia kuanzishwa kwa sheria yetu ya rushwa.

Tumefikia hatua nzuri katika kuandaa sheria hiyo, tumebakia kukamilisha ili ianze kutumika, tutayarekebisha kwa haraka ili suala hili la maadili wananchi waweze kutusaidia, kwani tunahitaji ushirikiano wao katika kulikamilisha suala hili.

Mhe. Spika, utawala bora ni sehemu muhimu sana katika kuendeshaji wa shughuli za serikali na hata taasisi binafsi katika zama hizi za mfumo wa siasa za ushindani wa uchumi unaozingatia soko. Nchi yetu katika kipindi cha miaka 10 iliyopita imeshuhudia hatua kubwa katika eneo hili.

Hivyo katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Umoja wa Kitaifa, itaendeleza jitihada za kukuza demokrasia na utawala bora. Serikali yangu itazingatia utawala bora wenye kuheshimu sheria, haki za binadamu, uhumu na wananchi kutoa maoni yao na kujieleza, inayojali usawa pasi na ubaguzi wa aina yoyote, iwe kwa sababu za kiitikadi za chama, dini au eneo analotoka mtu. Tutasimamia ujenzi wa demokrasia na utawala bora kwa kusimamia utekelezaji wa kazi na majukumu ya serikali kwa kuzingatia misingi ya demokrasia na utawala bora, kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Zanzibar iliyofanyiwa marekebisho ya 10 mwaka huu.

Vile vile nitaimarisha uwazi na uwajibikaji, nataka nirudie tena na kulifanya suala la uwajibikaji kuwa ni ajenda kitaifa. Serikali pia itaendelea kuimarisha Idara ya Mkurugenzi wa Mashtaka na kukamilisha hatua za wanasheria wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, kuendesha mashtaka katika ngazi zote za mahakama. Hatua hii imelenga katika kuhakikisha kuwa tunaondoa ucheleweshaji wa kesi pamoja na kurahisisha, kuharakisha na utoaji wa haki mahakamani.

Katika eneo hili la utawala bora serikali yangu pia itaimarisha Afisi ya Mkaguzi wa Mdhibiti wa Serikali Kuu, ili kujenga uwezo zaidi wa kiutendaji ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Lengo letu la kudhibiti na

kusimamia vyema mapato na matumizi ya serikali haliwezi kufanikiwa bila ya afisi hii kuwa na uwezo wa tija na kiutendaji. Tutahakikisha kwamba watendaji katika Afisi hii wanapata mafunzo kuhusu kada mpya ya ukaguzi ikiwemo ukaguzi wa thamani, ukaguzi wa kompyuta na ukaguzi wa mazingira, yaani *environmentary audit.*

Utawala bora unajumuisha uwazi na uwajibikaji. Katika kuhakikisha kunakuwa na uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma serikalini, katika kipindi kijacho nitahakikisha kwamba inajenga mazingira mazuri yatakayowawezesha watumishi wa serikali kutambua wajibu wao, kutekeleza na kufanya kazi kwa malengo na kupima matokeo ya kazi walizozifanya.

Kwa hivyo, suala la uimarishaji utendaji nikipe umuhimu wa kipekee, kwa vile hiyo ndio siri kubwa ya mafanikio ya majukumu haya tunayowaeleza wananchi. Lakini mbali ya kuhimiza uwajibikaji serikali yangu itaimarisha mazingira ya kazi, maslahi kama nilivyoeleza pale awali.

Katika kuimarisha Muungano wetu, nia yangu ni kutekeleza yale yote yaliomo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushughulikia mambo ya Muungano. Vile vile kuhusu kero za Muungano na changamoto ziliopo, tufanye kila jitihada kwa kushirikiana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili mambo hayo yanaendelea kujadiliwa kwenye kamati ya pamoja kuhusu Muungano yanafikia uamuzi wa haraka ili tuweze kupata maelekezo.

Katika kipindi kijacho yako mambo ya msingi ambayo tutapaswa tuyashughulikie.

1. Tutaimarisha utendaji wa kamati ya pamoja wa kutatua kero za Muungano, kwa kuandaa utaratibu madhubuti wa vikao vya pamoja vitakavyoendeshwa chini ya Wenyekiti wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mujibu wa taratibu ambazo zitakazofuatia baadae. Lengo letu ni utekelezaji wa haraka wa maamuzi yatakayofikiwa.

   Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndio inayoratibu mambo ya Muungano, naamini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itasimama kidete na kujitayarisha katika kuendeleza mazungumzo ya kamati ya pamoja pale nilipoachia mimi nilipokuwa Makamu wa Rais. Naamini Mhe. Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Mohamed Gharib Bilal, atakuwa ni kiongozi mahiri katika kuendeleza

jitihada zetu za kuyapatia ufumbuzi mambo ambayo tumeanza kuyazungumza ili yafikie uwamuzi wa mwisho.

2. Tutaimarisha uchangiaji na mgawanyo wa mapato wa mambo ya Muungano.

3. Tutaimarisha utaratibu wa kuandaa na kutekeleza mikakati na mbinu bora za kuinua uchumi wa pando zote mbili za Muungano.

4. Vile vile tutahakikisha kwamba taratibu za ajira za watumishi katika taasisi za Muungano zinashughulikiwa ili utumishi huo uwe na sura ya muafaka ya mambo ya Muungano.

Mhe. Spika, nchi yetu imekuwa na uhusiano mzuri na wa kuridhisha na nchi mbali mbali zilizo marafiki na mashirika ya maendeleo mbali mbali kwa kupitia njia ya moja kwa moja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Nachukua nafasi hii kuzipongeza nchi zote marafiki na mashirika mbali mbali ambayo yamekuwa yakitekeleza wajibu wake kwa kufanyakazi pamoja na Zanzibar, na kutusaidia pale ambapo misaada yao imeleta mafanikio makubwa kwetu. Nia yangu ni kuimarisha uhusiano huu kwa madhumuni ya kuendeleza ushirikiano katika juhudi zetu za kujenga nchi yetu na kuleta maendeleo.

Tutakuza ushirikiano wa karibu zaidi na mataifa mbali mbali na taasisi za kimataifa na taasisi nyengine zisizo za kiserikali kwa manufaa ya watu wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla.

Kuhusu uhusiano wa kikanda, tutahakikisha kwamba Zanzibar inashirikishwa kikamilifu katika taasisi za kikanda hasa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, na inapewa huduma na kufaidika na jumuiya hiyo.

Mhe. Spika, mwisho. Leo tumezindua Baraza la Nane la Wawakilishi. Hii ni siku ambayo itakumbukwa sana katika historia ya nchi yetu na taifa letu zima la Tanzania kwa jumla. Sura ya Baraza hili peke yake ni ya kujenga historia nzuri ya nchi yetu. Tunafungua ukurasa mpya katika muhimili huu muhimu wa nchi yetu. Najua kwamba Waheshimiwa Wajumbe wote mnafahamu na mnaelewa vyema kwamba matarajio ya wananchi na jinsi tutakavyowatumikia katika chombo hiki.

Aidha, naamini kwamba waheshimiwa nyote ni waumini wa maridhiano yetu ya kisiasa. Vile vile naamini kwamba mtayaendeleza maridhiano haya kwa lengo la kuendeleza nchi yetu, ili ipate mafanikio ya kiuchumi na kijamii kwa hali na mali.

Kwa mara nyengine tena natoa pongezi zangu za dhati kwako Mhe. Pandu Ameir Kificho, Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, kwa kuwa Spika tena wa kuliongoza Baraza la Nane la Wawakilishi la Zanzibar.

Namuomba Mwenyezi Mungu akuzidishie hekima na busara katika kuliongoza Baraza hili na ninataraji Waheshimiwa Wajumbe wote watakupa kila aina ya ushirikiano wao katika kuziimili na kuziendesha kazi zako kikamilifu.

Ni matarajio yangu kwamba vyama vyote vya siasa vilivyopo hapa nchini, jumuiya zisizo za kiserikali na wahusika wengine mbali mbali wote kwa pamoja watatumia fursa walizonazo katika kuwaongoza wanachama wao katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo kwa lengo la kuwapunguzia wananchi hao umaskini.

Watendaji wote wa serikali wa ngazi mbali mbali wataendelea kutimiza wajibu wao kwa ufanisi, tija na kwa nidhamu ya hali ya juu. Kwa wale watakaoteuliwa kushika dhamana mbali mbali, napenda niwatanabahishe kuwa wanachopewa wao ni dhamana na ni dhamana ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Kwa hivyo, tunawatarajia basi wajitume sana, tunawatarajia watekeleze majukumu yao kwa kujituma kwa nguvu zaidi, wafanye kazi zao kwa uadilifu, wafanye kazi zao kwa uhakika na kwa kuzingatia misingi ya usawa, umoja na mshikamano wa nchi yetu.

Mhe. Spika, nafahamu kuwa Baraza hili tukufu la Wawakilishi, linao wajibu mkubwa sana katika kuilinda na kuiletea nchi yetu maendeleo. Baraza hili linajukumu la kuchochea maendeleo, pia linawajibu wa jumla wa kusimamia serikali. Hivyo, Baraza litakapotekeleza wajibu wake kwa vizuri zaidi, ndio jinsi serikali itakavyoweza kutekeleza wajibu wake kwa mafanikio zaidi.

Kwa kuwa Baraza hili limeundwa kwa mchanganyiko, tena mchanganyiko mzuri sana baina ya wazoefu na vijana na kwa kuwa Baraza lina idadi kubwa ya zaidi ya wanawake kuliko Baraza lililopita na kwa kuwa utendaji wake unaendana na dhamira ya kuleta umoja wa kitaifa. Basi nina matumaini makubwa sana kwamba Baraza hili litatoa mawazo yaliyo bora zaidi kwa faida ya nchi yetu na watu wetu.

Mhe. Spika, namalizia kwa kusisitiza kwa mara nyengine tena kwamba Serikali ya Awamu ya Saba ya Umoja wa Kitaifa ninayoiongoza, itaongozwa kwa misingi ya haki na sheria na kufuata taratibu ziliopo na kufanyakazi kwa kuonesha mfano wa maadili mema na kuweka mbele maslahi ya Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe, kwa jumla hii ndio dira ya utendaji kazi wa Serikali ya Awamu ya Saba. Dira hii inaendana na malengo ya Mapinduzi yetu matukufu ya Januari 12 ya mwaka 1964 ya kuleta maisha bora na ustawi kwa watu wote wa Zanzibar. Amani, usalama na utulivu wa nchi ndio kiini cha mafanikio tunachotarajia. Nidhamu na kuheshimiana ndio ngao zetu, tutayalinda na kuyasimamia yote haya.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni sana kwa kunipa fursa hii adhimu ya kulitumia Baraza hili tukufu na kwa kupitia kwake kuweza pia kuwafikia wananchi na kuelezea masuala muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu na watu wake katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Ninafuraha sasa kutamka rasmi kwamba Baraza hili la Nane la Wawakilishi la Zanzibar nimelizindua rasmi *(Makofi).*

Mungu ibariki Zanzibar.

Mungu ibariki Tanzania.

Mungu ibariki Afrika.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza *(Makofi).*

Mhe. Spika: Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, Makamo wa Rais wa Kwanza Maalim Seif Sharif Hamad, Mhe. Jaji Mkuu wa Zanzibar Mhe. Hamid Mahmoud Hamid, Waheshimiwa Wajumbe, Waheshimiwa Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana.

Mhe. Rais, tunakushukuru sana kwa kukubali kuja hapa, umetenga muda wako na kuja kulihutubia na kulizindua rasmi Baraza hili, tunakushukuru sana *(Makofi).*

Hotuba yako Mhe. Rais iliyochukua kiasi ya muda wa saa 1:40 kulihutubia Baraza hili, imeanzisha ajenda ya mkutano ujao kuijadili hotuba hii na hatimaye kupokelewa rasmi na Waheshimiwa Wajumbe kama ilivyo kawaida kwa mujibu wa kanuni zetu.

Mhe. Rais kabla sijatoa shukrani za kufunga kikao chetu cha leo, naomba nimkaribishe mheshimiwa wangu mmoja ili atowe neno la shukrani kwa niaba ya Waheshimiwa Wajumbe, naye si mwengine isipokuwa ni Mhe. Abubakar Khamis Bakary.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti Dk. Ali Mohamed Shein, Mhe. Makamo wa Rais wa Kwanza, Mhe. Makamo wa Rais wa Pili, Mhe. Jaji Mkuu, Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu, Waheshimiwa Wageni wote mlioalikwa.

Mhe. Spika, ni wajibu wetu sote tuliopo hapa kumshukuru Mwenyezi Mungu wetu Mtukufu kwa kutujaalia kufika tena kwenye ukumbi huu tukiwa wenye afya na uzima. Pia tumtakieni rehema Mtume wetu Muhammad (SAW).

Mhe. Spika, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili kutoa maelezo mafupi ya shukrani kutokana na hotuba hii nzuri sana na iliyojaa hekima na kutoa mwanga kwa Zanzibar yetu. Zanzibar yetu mpya ambayo ndio Zanzibar tunayoitaka. Hotuba hii Mhe. Spika, naamini itakuwa ni moja ya zana zetu katika ujenzi wa Zanzibar mpya.

Mhe. Spika, tarehe 05/11/2009 aliyekuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Aman Abeid Karume, alikutana na Katibu Mkuu wa CUF huko Ikulu na kuridhiana juu ya mustakabali wa nchi. Sote tumeshuhudia kwa jiwe hili la umoja lililotupwa na viongozi hawa wawili katika dimbwi la amani na utulivu, limezaa cheche za mshikamano. Pia limezaa cheche ya amani na utulivu katika pembe zote za Zanzibar.

Mhe. Rais wa Zanzibar tunakushukuru sana kwa kuendeleza mshikamano huo na kitendo chako hiki cha leo kinatoa ujasiri mkubwa zaidi ambao umetupa changamoto sisi wawakilishi wako.

Napenda nichukuwe fursa hii kwa niaba ya wawakilishi wenzangu, tukuhakikishie kwamba sisi sote wawakilishi tuliomo humu bila ya kujali tofauti zetu, tutakuwa ni askari madhubuti wa kulinda matunda haya.

Mhe. Rais, uzalendo wetu, umoja wetu na kuaminiana kwetu ambako tumeuonesha ulimwengu miezi michache iliyopita ndio silaha yetu Wazanzibari. Hata bwana Abraham Linkon aliyekuwa Rais wa Marekani, aliwaasa wananchi wake huko Ilinois mwaka 1858 kwa kusema yafuatayo, naomba ninukuu.

> "Nyumba iliyogawika kamwe haiwezi kusimama".

Hapa bwana Linkon alikuwa akihubiri umoja, amani na utulivu ndani ya Marekani. Nakweli kuungana kwao na umoja wao ndio uliolifanya taifa la Marekani kuwa na nguvu kubwa hadi hii leo.

Mhe. Rais, somo hili zuri ambalo na wewe umelisisitiza katika hotuba yako ya leo, tutalitekeleza kwa vitendo siku zote katika kazi zetu za uwakilishi ndani ya Baraza, nje ya Baraza na majimboni kwetu.

Mhe. Rais, tarehe 05/08/2010 jengo hili jipya la Baraza lilifunguliwa na tarehe 09/08/2010, sisi wawakilishi wako tuliomo humu Barazani tuliweka historia kubwa katika nchi yetu, kwa kuirekebisha katiba ya Zanzibar kuwa sasa ni katiba ya kujenga umoja, mshikamano na maendeleo.

Jaji Sowa wa Ghana mwaka 1980 alielezea jinsi ya katiba nzuri ilivyo kwa kusema mambo yafuatayo, naomba ninukuu.

> "Katiba nzuri ni ile inayowaunganisha wananchi wake, inayoleta umoja na ushirikiano, inayowaonesha wananchi njia nzuri za maendeleo yao na inayowawekea misingi ya sheria na ambayo inaweza kuhimili misukosuko ya kisiasa na kijamii".

Jaji huyo alisema kuwa Katiba hizi ni chache duniani. Mhe. Rais kwa sababu Katiba yetu ya Zanzibar imekidhi yote hayo, basi nathubutu kusema kwamba Katiba ya Zanzibar sasa imekuwa ni miongoni mwa Katiba nzuri na zilizobora ulimwenguni. *(Makofi)*

Kwa hivyo, sote tujipongezeni kwa hili na tunakuhakikishia sana Mhe. Rais kwamba sisi Wawakilishi wako tutailinda Katiba hiyo kwa vitendo kwa wakati wote. *(Makofi)*

Mhe. Rais, nakumbuka Kiongozi mmoja wa Ujerumani alipowaasa mahakimu wake wakati wa kufungua jengo moja la mahakama, kuwa angependa kwa wanaodai pamoja na wadaiwa wote wanaotoka katika jengo hilo watoke wakiwa wamefurahi.

Tunakushukuru sana Mhe. Rais na wewe kwa kutuasa sisi Wawakilishi tutakaokuwemo humu katika kipindi hiki cha miaka mitano, kwamba tulifanye jengo hili la Baraza la Wawakilishi kuwa ni ngome ya kuwalinda na kuwatetea wananchi na kufanya chachu ya maendeleo. *(Makofi)*

Wasia wako huo Mhe. Rais tutaufanyiakazi sana na kwa nia ya kujenga na kuzidisha umoja wetu.

Mhe. Rais, wakati Mhe. Rais Regan akiapishwa tarehe 20 Januari, 1981 alisema yafuatayo. Naomba kunukuu.

> "Ni lazima tujue kwamba sumu na silaha za hatari katika dunia hii kamwe haishindi silaha ya umoja na ujasiri wa wananchi".

Kwa hivyo, kama ulivyotuusia wewe Mhe. Rais kwamba umoja ni nguvu na unashinda kitu chochote kile, basi haya tutayatekeleza kwa vitendo. *(Makofi)*

Mhe. Rais, mwisho ninapenda niseme kwamba Mtume wetu Muhammad *(S.A.W)* amemaliza maneno yote haya kwa kunakiliwa na Abuu Ghuraira kwa kusema yafuatayo.

> "Mwenyezi Mungu hamtizami mtu kwa umbo lake, mwili wake au uzuri wake, isipokuwa anachokitizama ni moyo wake, imani yake pamoja na nia yake".

Kwa maana hiyo, tunachosisitizwa hapa ni nia njema, ukweli, umoja pamoja na nia ya kujenga. Kwa hivyo, tushikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu na *Inshaallah* atatutilia baraka na kutuzidishia maendeleo kwa Zanzibar yetu pamoja na vizazi vyetu. Amin.

Mwisho Mhe. Rais, tunaomba tena kwa niaba ya wenzangu wote, tunakushukuru sana kwa hotuba yako nzuri na pia tunakutakia kila la kheri, afya njema wewe na familia yako, ili uzidi kutuelekeza katika safari yetu hii refu tuliyoianza hivi karibuni ya kuleta umoja, udugu na maendeleo kwa Zanzibar na vizazi vyake.

Mungu Ibariki Zanzibar.

Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Rais, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Ustadhi wangu huyu Mhe. Abubakar Khamis Bakary, maana leo hii ametutolea na kipande mbali ya *quotations* na *citation* za viongozi mbali hasa wa Marekani. Kwa hivyo, nimshukuru kwa neno hilo la shukurani alilolitoa, kutokana na hotuba yako nzuri uliyoitoa hapa Baraza la Wawakilishi.

Waheshimiwa Wajumbe, nichukue nafasi hii kumshukuru tena Mhe. Rais kwa kutoa hotuba yake nzuri sana, ambapo kama nilivyotangulia kusema hapo kabla kwamba imeanzisha ajenda ya shughuli zetu za Mkutano ujao wa Pili wa Baraza hili la Nane, kwenye siku itakayotolewa baadaye kesho. Kwa kweli hotuba yako Mhe. Rais ndio dira yetu ya kuanzia kazi.

Kwa hivyo, bila ya shaka nitaiomba afisi yake itupatie nakla hiyo ili turuhusu wajumbe wote wapate, kwa ajili ya mjadala wa mkutano wetu ujao.

Mhe. Rais pamoja na Waheshimiwa Wajumbe, nichukue nafasi hii kukushukuruni na nyinyi kwamba muda wote Mhe. Rais wakati alipokuwa akitoa hotuba yake tulikuwa watulivu, wasikivu na hapana shaka hotuba hiyo tumeielewa vizuri mno.

Vile vile nawashukuru wageni wetu waliopo pale juu na wengine walioko kwenye eneo la hapa chini na pia kuwa wasikivu na watulivu kwa muda wote, ambao Mhe. Rais alikuwa akitoa hotuba yake katika ukumbi huu.

Mhe. Rais shughuli hii isingenoga vizuri bila ya kuwepo Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad. Kwa kweli huyu ni Mwalimu wangu, ingawa hakunifundisha lakini alikuwa Mwalimu wakati nilipokuwa nikisoma pale Skuli ya Lumumba, kwa hiyo ni Mwalimu wangu. Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais nakushukuru sana kwa kushirikiana nasi kwenye shughuli ya leo na kukubali kuungana na Mhe. Rais kwenye shughuli hii. *(Makofi)*

Mhe. Hamid Mahmoud Hamid Jaji Mkuu wa Zanzibar nawe pia nakushukuru sana, kwa muda mrefu umekuwa unashirikiana nasi kwenye shughuli kama hizi na wakati mwengine nakupa *notice* ya muda mfupi sana. Lakini bado kwa uzalendo wako unakubali kuja kushirikiana nasi, ili kunogesha shughuli zetu. *(Makofi)*

Hali hii ni maalum kwa shughuli za Baraza kama hili, kwa sababu leo hii kama vile inavyokuwa kwa siku nyengine za aina kama ya leo, ile mihimili mitatu ya mgawanyo wa madaraka kwa mujibu wa Katiba yetu ya Zanzibar na hata ilivyo katika nchi nyengine yoyote leo ipo hapa. *(Makofi)*

Executive ndio hii hapa, *Legislature* ndio mimi na nyinyi wenzangu na *Judiciary* ndio hii hapa. Kwa hiyo, leo wananchi wa Zanzibar wamewakilishwa vizuri sana na mihimili yote ya Dola yetu ya Zanzibar. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, shughuli yetu ya leo kwa mujibu wa orodha ya shughuli zetu, ilikuwa kwa ajili ya Mhe. Rais tu kuja kutoa hotuba yake pamoja na kulizindua Baraza na tayari ameshafanya kazi hiyo. Kwa hivyo, kimsingi shughuli zetu za leo zimemalizika, imebakia shughuli nyengine lakini hiyo itafanywa kesho, ambayo ni kubwa tena ni muhimu.

Kutokana na umuhimu wake ndio tumeiweka mwisho makusudi, ili Waheshimiwa Wajumbe mpate kunong'ona nong'ona kati yenu na hata na mimi mkininong'onesha kidogo nitakubali kunong'ona nanyi. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Rais, shughuli ya kesho ni kuwachagua Wajumbe wa Baraza hili watano, ambao wataungamana na wenzao katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakima kama ni Wawakilishi wa Baraza hili ndani ya Bunge hilo. *(Makofi)*

Katika hilo naamini pande zote mbili tayari zimeshamaliza Makamo wa Pili wa Rais jana aliongoza timu yake, kwa ajili ya kupata mapendekezo ambayo yatapigiwa kura kesho hapa, kwa upande wa Chama cha CUF wajumbe wake sijui kiongozi ni nani kwa mara hii, aa! Kumbe yupo hapa Mhe. Abubakar Khamis Bakary naye naamini ameshamaliza kazi hiyo. Kwa kweli Mhe. Rais, wajumbe watano tumewagawa kwa utaratibu maalum kwa mujibu wa kila chama chenye wajumbe humu ndani kipate nafasi katika viti hivyo.

Kwa hivyo, kwa upande wa Chama cha Mapinduzi wao wanao wajumbe watatu wakupeleka pale Bungeni ni chama chako hicho Mhe. Rais, Maalim nawe unao wa kwako wawili ambao wataingia Bungeni. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, kazi tayari imeshamalizika na naamini Katibu ndiye Mkurugeni wa Uchaguzi wa ndani hapa na hata jana aliniapisha yeye na mimi ndio nikapata nguvu ya kuwaapisha wenzangu hawa. Kazi zote matayarisho yake yalikamilika na kazi ya uchaguzi wa wabunge hao kesho itamalizika Mwenyezi Mungu akipenda *Inshaallah*.

Baada ya hayo machache nitoe taarifa kwamba kutakuwa na picha ya pamoja hapo nje kama nilivyotangulia kusema, kwamba meza kuu hapa tutatoka tutakaa pahala kidogo kwa ajili ya kupumzika, wakati waandaaji wa eneo la kupiga picha ya pamoja wanatayarisha hilo.

Kwa hiyo, picha hiyo itakuwa viongozi pamoja na nyinyi kwa utaratibu wa wajumbe 20 na baadaye 20 mpaka kumalizika, picha nyengine zitaongozwa na mtumishi wetu mmoja atakayeeleza.

Vile vile kwa upande wa wake wa viongozi waliopo pale juu watajumuika nasi katika picha hiyo na tunawaomba nao waelekezwe pale tutakapopumzika sisi, ili baadaye tutoke kwa pamoja. Kwa hiyo, wale wasaidizi wao tunawaomba sana wawalete katika chumba cha mapumziko kwa ajili ya kujiandaa kwa picha hiyo ya pamoja. *(Makofi)*

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi nakushukuru sana kwa kufanyakazi kubwa, ambayo ipo kwa mujibu wa taratibu za Kanuni na Katiba pia inakuruhusu chini ya ibara ya 84 wakati wowote utakapoona inafaa, unao wasaa na unalo neno la kuwaambia Waheshimiwa Wajumbe hawa, basi nipe taarifa tu na mimi nitakwambia sawa karibu.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo sasa naahirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 12 Novemba, 2010 saa 3:00 za asubuhi, ili tuendelee na shughuli zetu.

Ahsanteni sana.

(Saa 6:24 mchana Kikao kiliahirishwa mpaka tarehe 12/11/2010 saa 3:00 asubuhi)